**MAJALIWA** atoa msimamo wa serikali walimu astashahada

UKURASA 3



**MWINYI:** Zanzibar ni mahali salama utalii wa mikutano na makongamano

UKURASA 3

**SUMAJKT** kutekeleza miradi ya Comoro

UKURASA 7


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 13, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581828

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**VAN DIJK ALIA NA KADI NYEKUNDU YA KWANZA**

UKURASA 22

## ALIKO ASKOFU MUNGA

# Polisi yavunja ukimya

**BAGONZA** atoa angalizo...

*Endelea ukurasa wa 2*



Askofu Dk.Steven Munga



**RIPOTI MAALUM**

## Ulaji chipsi ulivyobadili utaratibu wa mlo kamili

UKURASA 4



# Samia: Uchaguzi Serikali za Mitaa fursa ya maendeleo

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YASAKA USHINDI KISASA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia: Uchaguzi Serikali za Mitaa fursa ya maendeleo

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wananchi kutokupuuzia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, watumie fursa hiyo kugombea na kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Samia ametoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi mkoani Mwanza, akielekea Geita kwa ajili ya kufunga maonesho ya teknolojia ya madini.

Alisema, ili kufanikisha hatua hiyo, inabidi wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, pamoja na lile la serikali za mitaa hususani wale ambao tayari wamefikisha umri wa miaka 18.

Alisema anatarajia kurejea mkoani humo, kushiriki na Watanzania kuadhimisha Kilele cha Mbio za Mwenge Kitaifa, kitakachofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba Oktoba 14, mwaka huu, yakitanguliwa na kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

"Kilele cha mbio za Mwenge kitaifa kinatimiza miaka 60 ikiambatana na miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kuanzishwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Polisi vyote kwa pamoja vimejenga historia ya kutimiza miaka 60 mwaka huu," alisema.

Alisema ifikapo Novemba 27, mwaka huu, ni siku ya kupiga kura ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa na vitongoji, hivyo kila mwananchi anatakiwa kujitokeza kutekeleza haki yake ya msingi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, wakati akitoa salamu kwa niaba ya wananchi wake, alisema serikali ilitoa zaidi ya Sh. trilioni tano kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati iliyoko mkoani humo.

Aliwaomba wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi katika kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa , kwani mkoa umepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo.

Wakati huo huo, vyama vya siasa visivyopata ruzuku serikali vimeomba kupatiwa, ili kushiriki uchaguzi kama vilivyowezeshwa mwaka 1995.

Wamesema ni muhimu kutafuta utaratibu, ili kuwezeshwa kushiriki katika uchaguzi huo muhimu.

Kauli hiyo iliyolewa jana, jijini Dodoma, mara baada ya kumaliza mkutano wa dharura wa Baraza la Vyama vya Siasa ambapo washiriki walipatiwa mafunzo kuelekea uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema kuna vyama 19 vilivyosajiliwa, lakini si vyote vina uwezo wa kushiriki katika uchaguzi kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha.

"Tumekubaliwa hapa kuwa ni muhimu kutafuta utaratibu vyama viweze kuwezeshwa kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa," alisema.

Alisema wameomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iwapatie orodha ya vijiji, vitongoji na mitaa, kwa kila chama na iwekwe katika tovuti ya kila halmashauri.

Alisema kama TAMISEMI itazingatia maoni yao kutakuwa na uchaguzi bora na kuomba yasijirudie yaliyotokea katika uchaguzi kama huo, uliofanyika mwaka 2019.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, alisema ni muhimu ikatolewa ruzuku kusaidia gharama za uchaguzi, ili kuongeza ushindani.

"Chama tawala hakiwezi kufanya uchaguzi peke yake, ni muhimu vyama vingine navyo viwafikie wananchi, ili kuwahamasisha, kuweka mawakala, mihuri na gharama nyingine," alisema.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema uchaguzi ni gharama na vyama havina fedha, hivyo serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha vinashiriki uchaguzi kama ilivyofanyika mwaka 1995 ambako wagombea wote waligharamiwa na serikali.

"Hoja hii tumeijadili haijapata majibu, lakini imechukuliwa, tunategemea itapata majibu baadaye. Nimetoa tahadhari kwa serikali kwamba, ina wajibu wa kuhakikisha vyama vyote vinashiriki uchaguzi , kwa kuwa ukiviachia vyama vijiendeshe vyenyewe nani anawajibika kutafuta fedha za uchaguzi katika chama peke yake?,"

"Vipo vyama vichache vinapata ruzuku kidogo, lakini kuna vyama vingi havipati hata hiyo ruzuku, ukitegemea vikashindane kwa usawa, tunakuwa hatutendi haki," alisema.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema: "Mambo makubwa matatu ambayo tunaamini TAMISEMI watafanyia kazi ni suala la uapishaji mawakala, tumejenga hoja ni vizuri waapishwe ngazi za vijiji, badala ya utaratibu uliotumika hivi sasa katika ngazi ya halmashauri, kwamba wakusanywe ngazi ya kata au halmashauri husika," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alivitaka vyama hivyo kutotumia lugha za matusi, kashfa, uchochezi au vitendo vitakavyovuruga amani katika uchaguzi huo.

Alisema vyama vinapaswa kufanya siasa za kistaarabu wakati wa kampeni za kuwanadi wagombea wao.

"Lengo la mafunzo haya ni kuwakumbusha kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika kipindi mtakapokuwa mnajinadi kwa wananchim, ili kuwashawishi waamini na hatimaye kuwachagua wawakilishi kutoka katika vyama vyenu.

"Kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo tusije kudhani kila kitu kwetu ni uchaguzi pekee, amani na umoja wa taifa ni muhimu zaidi kuliko hata huo uchaguzi. Amani ikikosekana hata fursa tutakayopata ya kushiriki uchaguzi haitakuwapo," alisema.

**IMEANDALIWA na Remmy Moka (MWANZA) na Augusta Njoji (DODOMA)**

# Polisi wavunja ukimya taarifa za Askofu Munga kukamatwa

**Na Oscar Assenga, TANGA**

JESHI la Polisi limekanusha taarifa za kukamatwa kwa Askofu mstaafu wa Dayosisi ya KKKT Kaskazini Mashariki, Dk. Stephen Munga, ambazo zimeenea katika baadhi ya mitandao ya kijamii kwamba kongozi huyo anashikiliwa na jeshi hilo.

Akizungumza jana na Nipashe, iliyotaka kujua ukweli kuhusu taarifa hizo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Muchunguzi, alisema kiongozi huyo wa dini mstaafu hashikiliwi na jeshi hilo.

Katika taarifa ya Askofu Emmaus Mwamakula, aliyoandika kwenye ukurasa wa kijamii wa Facebook, alidai kwamba aliongea na Askofu Munga akiwa kituo cha polisi kutaka kujua tuhuma zake, lakini hawakuwa na uhakika kwani ilisemekana ni tuhuma za kughushi nyaraka alipokuwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Tanga.

Alisema kwamba Askofu Munga, ni miongoni mwa maaskofu watetezi wa haki na kwa sababu ya misimamo yake isiyoyumba, "amelipa gharama kubwa sana na kupata misukosuko mingi na miaka ya hivi karibuni aliwahi kuugua ugonjwa wa ajabu na katika mazingira ya kutatanisha sana, ilibidi akimbizwe Afrika Kusini, ndiko ambako aliponea."

Alisema wanalifuatilia kwa umakini suala hilo na watAujulisha umma kwa kila hali.

Askofu wa Dayosisi ya Karagwe ya KKKT, Dk. Benson Bagonza, pia aliandika katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Facebook, kuwa "Polisi wameletewa". Andishi la Askofu Bagonza lilikuwa kama ifuatavyo:

**POLISI WAMELETEWA**

**1.** Unapopelekwa polisi na mtu ambaye ndiye angekudhamini kama ungekamatwa na polisi kwa kosa lolote - usihangaike kutafuta dhamana.

**2.** Unapopelekwa kwa mtu ambaye ndiye angeletwa kwako umsaidie; ujue viwango vya ustahimilivu vimeyumba. Aliyepeleka, aliyepelekewa na aliyepelekwa wako msalabani. Hekima itawale - matumizi ya mamlaka, madaraka havina nafasi.

**3.** Tumezoea kuona Dola ikitumia dini kwa mikakati ya kisiasa. Ukiona dini inatumia Dola katika mikakati yake ujue chumvi imechacha. Dini ikikosa ushawishi ni hatari kuliko sumu na bangi. Muuzeni askofu, ili madeni yalipwe na tukomboe mali zinazouzwa.

**4.** Kiongozi wa kweli wa dini afurahie kupelekwa Polisi na hata kwa Pilato. Yeye si wa kwanza. Alitangulia Bwana Yesu Polisi na kwa Pilato. Alikutwa na hatia isiyo hatia. Hatia isiyo hatia humwendea aliyepeleka na aliyepelekewa. Yesu alipopelekwa na kuhukumiwa, ulimwengu uliokolewa. Askofu akidhalilishwa, madeni yatalipwa?

**5.** Jinsi unavyomshughulikia mstaafu yeyote ndivyo unavyowafundisha wasaidizi wako namna ya kukushughulikia utakapostaafu. Polisi msinunue kesi isiyo na bei. Ya sirini yakiletwa hadharani, ya hadharani yataenda sirini.

Nawatetea polisi kwa sababu wameletewa mzigo. Sema tu, mizigo mingine ni kama ya dawa za kulevya. Ukikamatwa nao, unakusumbua wewe.



HABARI KITAIFA

# Majaliwa atoa msimamo wa serikali walimu wenye astashahada

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali haijatoa maagizo ya kuwaondoa kazini walimu wa cheti, bali imewataka watumie mpango wa mafunzo endelevu kazini kwenda vyuoni kusoma.

Amesema serikali imefanya maboresho ya sera na mitaala ya elimu nchini, ambayo pamoja na mambo mengine, imeleta mabadiliko katika sifa za chini za mwalimu katika shule za msingi kuwa na stashahada (diploma).

"Pamoja na mabadiliko haya, serikali inatambua kuwa bado wapo walimu ambao hawajafikia sifa ya kuwa na stashahada au diploma na hakuna agizo la kuwataka waondolewe katika ajira," amesema.

Alitoa kauli hiyo juzi Oktoba 11, mwaka huu, wakati akizungumza na mamia ya walimu na wadau walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, yaliyofanyika kwenye uwanja wa mpira wa shule ya sekondari Ushirombo, wilayani Bukombe, mkoani Geita.

Alisema walimu wote ambao hawana sifa ya stashahada au diploma watumie fursa ya mpango wa mafunzo endelevu kazini kwenda vyuoni kusoma, ili kupata sifa ya diploma au kujiendeleza kupitia moduli kwa mfumo wa LMs - Learning Management System chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).

"Kupitia mfumo huu, serikali imeingia makubaliano na kampuni ya simu ya Airtel, kwa walimu wenye vishikwambi na wanatumia mtandao wa Airtel kupakua moduli bure kwa ajili ya kujiendeleza," alisema.

Waziri Mkuu pia aliagiza TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, taasisi za elimu, sekta binafsi na wadau wa sekta ya elimu nchini, wahakikishe walimu wanajengewa mazingira bora ya kazi, ili watimize majukumu yao kwa ufanisi.

Pia aliwataka waimarishe programu za mafunzo kwa walimu, ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, huku akiwataka waajiri kuwapa mafunzo walimu pamoja na taasisi zinazohusika na udhibiti wa ubora waendelee kutimiza majukumu yao.

Katika kuboresha sekta ya elimu nchini, Waziri Mkuu alisema serikali imeendelea kuboresha na kusimamia miundo ya watumishi wakiwamo walimu.

"Serikali imeboresha stahiki za msingi za watumishi kwa kupandisha madaraja na kuhakikisha wanapata nyongeza ya mishahara yao kwa wakati," alisema Majaliwa.

Akiainisha maboresho mengine, Waziri Mkuu alisema: "Serikali imeimarisha miundombinu mahali pa kufanyia kazi, ikiwamo kuhakikisha kuna madarasa, maabara, mabweni, majengo ya utawala na sasa tumeingia kwenye ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na kuimarisha ajira zao."

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari, kupitia miradi mbalimbali kama vile Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), Mradi wa Kuimarisha na Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST), Mradi wa Huduma za Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira (SWASH), Programu ya Uboreshaji Kada ya Ualimu (GPE-TSP) na Programu ya Kutekeleza Elimu kwa Matokeo (EP4R).

Akielezea kuhusu upandishaji madaraja kwa walimu, alisema: "Kati ya Machi, 2021 na Agosti, 2024, walimu 601,698 nchi nzima wamepandishwa madaraja na serikali imetumia Sh. trilioni 1.3 kuwalipa. Na niwatake maofisa elimu kuwatembelea walimu vijijini na kusikiliza kero zao," alisisitiza Waziri Mkuu.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi sasa, serikali imebadilisha kada/miundo jumla ya watumishi 36,768 kwa gharama ya sh. 3,090,476,931.00 na imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 144,356 ya Sh. milioni 229.9.

Akimkaribisha Waziri Mkuu, kuzungumza na hadhara hiyo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko aliwashukuru walimu wa Tanzania, kwa kuendelea kuiheshimisha taaluma yao na kuwa chanzo cha maarifa kwao, hivyo wailinde kwa wivu mkubwa taaluma hiyo. Dk. Biteko alisema mwaka 2015 wakati anachaguliwa kuwa mbunge, wilaya yake ilikuwa ikishika nafasi ya mwisho katika mitihani ya taifa.

"Nilizungumza na walimu kuhusu matokeo mabaya na wakasema tusiwaache walimu nyuma, hivyo tulianza kukutana na kufanya tathimini na sasa tunafanya vizuri," alisema.

Alisema viwango vya ufaulu vimekuwa vikiongezeka kila mwaka, huku akitolea mfano wa matokeo ya mwaka jana kwamba darasa la saba ya wilaya hiyo ilishika nafasi ya pili katika mkoa huo, darasa la nne ilipata wastani wa asilimia 78 na kuwa nafasi ya pili kimkoa.

"Kidato cha pili tulikuwa na ufaulu wa asilimia 98, kidato cha nne ufaulu ulikuwa asilimia 96, kidato cha sita ulikuwa asilimia 100 na hizi zote tulikuwa wa kwanza. Katika mitihani ya 'mock' ya kanda ambayoilijumuisha mikoa mitano yenye Halmashauri 37, Wilaya ya Bukombe tumeshika nafasi ya tatu, tukiwa nyuma ya Ilemela na Nyamagana. Hivyo, nilione tutenge siku moja ya kusema asante mwalimu," alisema.

Aidha, Dk. Biteko amesema kuwa walimu nchini wasivunjike moyo, waendelee kufanya kazi yao na kwamba maisha yao ni kielelezo cha mafanikio katika taifa na kuwa wao ni nyota inayoangaza na yeye ataendelea kushirikiana nao.

Katibu wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), Mkoa wa Geita, Pauline Tinda, alisema tangu mwaka 2019, Wilaya Bukombe imekuwa ikiadhimisha Siku ya Mwalimu ambayo inalenga kutekeleza maelekezo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuwatambua na kutoa tuzo za umahiri, kwa walimu wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha masomo ya kusoma, kuandika na kuhesabu. Aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha utendaji kazi kwa walimu ma ustawi wa walimu kwa kufanya jitihada mbalimbali, ikiwamo kuwapandisha madaraja. Pia alimshukuru Dk. Biteko kwa kuendelea kuthamini mchango wao katika jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kuwa benki hiyo inatambua umuhimu wa walimu nchini na kuwa watu wengi wamefanikiwa kutokana na mchango wao.

"Sisi tunawapongeza walimu wote nchini. Tumeendelea kuunga jitihada nzuri zinazofanywa, ili mwalimu awe na mazingira mazuri ya kufanya kazi. Hadi sasa tumetoa zaidi ya shilingi bilioni moja, ili kununua madawati na leo (jana) tunachangia madawati 545 na magodoro 88 kwa shule mbalimbali za wilaya hii, ili kusaidia elimu ya Tanzania iwe bora zaidi," alisema.

# Mwinyi: Zanzibar ni nchi salama kwa utalii wa mikutano na makongamano

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar ni nchi salama kwa utalii wa mikutano na makongamano ya kimataifa.

Alhajj Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana, wakati wa kongamano la kwanza la Kiislam la kimataifa lililowakutanisha pamoja mashehe mbalimbali kutoka mataifa 18 duniani kwenye viwanja vya New Amani Complex, wilaya ya Mjini, mkoa wa Mjini Magharibi.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ina fursa kubwa ya kukuza utalii wa maadili 'Halal Tourism' kama chanzo cha mapato na ajira kwa watu wake, kupitia kongamano hilo la Kiislamu la kimataifa, limetoa mwangaza kwa nchi kama sehemu ya utalii wa Maadili hasa kwa wageni wanaofika kuitembelea, sio tu kujifunza dini lakini kufurahia uzuri wa mandhari na haiba ya nchi, mila, silka, utamaduni na ukarimu wa watu wake.

Akizungumzia faida za kongamano hilo, Alhajj Dk. Mwinyi alibainisha kuwa haziko za kiimani pekee, bali pia kuna manufaa makubwa ya kiuchumi kwa Taifa.

Pia alieleza mafanikio ya tukio hilo muhimu kwa Zanzibar, ni ufunguo adhimu wa kuitangaza kwa utalii wa maadili "Halal Tourism", ambao watu kutoka sehemu mbalimbali duniani huja kushiriki mikusanyiko ya kidini na matukio yenye uhusiano na tamaduni za dini.

Alisema ni jambo la kujivunia na kumshukuru Mwenyezi Mungu kuona wageni wengi kutoka mataifa tofauti duniani, wameungana kupitia mitandao ya kijamii kuangalia moja kwa moja kongamano hilo muhimu.

Alhajj Dk. Mwinyi aliwahakikishia wananchi wa Zanzibar kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa mikusanyiko kama hiyo na kuunga mkono jitihada za taasisi binafsi, ikiwamo kukuza uchumi na maadili ya nchi, ili kupatikane jamii yenye maadili na kuiweka nchi kwenye hadhi ya utalii wa maadili ambao hivi sasa umeshika kasi duniani.

Aliiasa jamii kuendelea kudumisha maadili kwenye maisha yao ya kila siku, ili kujenga taifa lenye maelewano, amani, heshima na ushirikiano kwa wote. Hatua hiyo akisema ina mchango muhimu katika kupatikana kwa mafanikio duniani na kesho mbele ya haki.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisifu amani iliyopo nchini na kueleza utulivu wa watu wake kutokana na ukarimu na maadili haya walivyooonesha kwenye kongamano hilo.

Akihadhir mbele ya zaidi ya waumini wa Kiislam na waananchi wa Zanzibar 20,000 waliofika viwanja vya New Amani Complex, kumshuhudia Mufti Mkuu wa Zimbabwe, Ismael Menki, alisema maendeleo kwa taifa lolote duniani hayatimii pasi na kuwapo ustawi wa amani na usalama kwa nchi na watu wake kwa kuendeleza, kudumisha umoja, upendo na kuheshimiana miongoni mwa jamii.

Mufti Menki alisisitiza mshikamano miongoni mwa jamii na kuwasihi waendelee kufungamana kwa Imani, heshima na upendo sio kufarakana kwa tofauti za mitazamo ya dini na siasa.

Pia aliwasisitiza waislamu kuzingatia zaidi utulivu wanapokuwa kwenye sala zao kwani kufanya hivyo ni kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu (S.W), vilevile alipongeza maendeleo makubwa yaliyofikiwa Zanzibar akitoa ushuhuda wa tofauti ilivyo sasa na miaka 10 iliyopita, ikiwa mara ya kwanza kufika Zanzibar wakati huo.

Wakizungumza kwenye Kongamano hilo, Sheikh Ali Hamuuda Ali kutoka Uingereza, Sheikh Wael Ibrahim kutoka Australia na Dk. Muhammad Salah, Sheikh kutoka Misri, walisisitiza wananchi wa Zanzibar kuendelea kutunza amani na usalama kwa ustawi wa nchi yao, hasa katika kuzifikia ndoto za maendeleo ya taifa lao.

Walieleza uwapo wa amani na utulivu wa nchi husaidia hufanikisha mazuri yasiyowezekana, kuwezekana kwa usatawi mzima wa jamii.

Aidha, mashehe hao pia walihimiza kuhusu kuzikimbia dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa kutofanya matendo yatakayomkosea Allah (S.W) pamoja na kujiepusha na anasa zinazomchukiza, Mwenyezi Mungu.

Eneo lingine waliloligusia masheikh hao ni kusisitiza waislamu kusalimiana kwa upendo na kushirikiana kwa hata wasiokua waislam, ili kujenga jamii moja yenye usawa, upendo, kuheshimiana kwenye kujenga maendeleo ya nchi yao, pamoja na kuwahimiza kudumisha sala za usiku katika kujitakasa na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu (S.W), ili kujiepusha na maovu yanayotokana na sheitwani na kujitakasa kwa Allah (S.W).

RIPOTI MAALUM

# Ulaji chipsi ulivyobadili utaratibu wa mlo kamili

Na Waandishi Wetu



Wateja wakisubiri huduma kutoka kwa muuza chipsi eneo la Jiwe la Mkapa, Kisesa wilayani Magu, mkoa wa Mwanza, hivi karibuni. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

CHIPSI kuku, chipsi yai au chipsi mishkaki kimekuwa chakula maarufu miongoni mwa watu wa marika yote. Si kinababa, kinamama, vijana wa kike na wa kiume.

Ulaji wa aina hiyo ya chakula, umetajwa kubadili matumizi ya chakula bora na mlo kamili, kwa sehemu kubwa ya familia nchini pamoja na mtu mmoja mmoja.

Awali, ulaji wa chakula hicho ulionekana kukithiri zaidi Dar es Salaam, ukaenea hadi miji mikubwa na midogo na sasa hadi vijijini umejipatia umaarufu.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe Jumapili, umebaini sehemu ya kubwa ya familia za mikoa ya Kanda ya Ziwa, zinatumia chakula hicho kama sehemu ya milo mitatu na kusahau utaratibu wa mlo uliozoeleka kama vile ugali na wali, kwa kula pamoja na nyama, samaki, mboga na maharage.

Mkoani Kagera, baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe, akiwamo Rozalia Mjumba, mfanyabiashara wa Soko Kuu la Bukoba, anasema kubanwa na majukumu ndiyo sababu ya kugeukia chakula hicho.

Anasema kutokana na kubanana na shughuli mbalimbali katika kazi zake, hulazimika kuagiza chipsi na wakati mwingine kuondoka na chakula hicho kwenda nacho nyumbani, kwa ajili ya familia yake. Anasema muda anaotoka kazini, anakuwa hana uwezo tena wa kuandaa chakula kingine.

"Chakula changu ninachokipenda zaidi ni chipsi iliyochanganywa na yai. Inakuwa na gharama kidogo Sh. 2,500. Nikinunua na pepsi ni 3,000 jumla ambayo naiona hainigharimu sana. Lakini nikiwa nyumbani, wakati mwingine naweza kula wali au ugali na mboga za majani, nyama au samaki. Ninapopata muda wa kuandaa chakula hicho," alisema.

Mjumba ambaye ni mkazi wa Kata ya Miembeni, Manispa ya Bukoba, anasema wakati mwingine hata akiwa nyumbani, anaagiza bodaboda kumpelekea chipsi, kwa ajili yake na familia ya watoto watatu, kwa kwa kuwa ndicho chakula wanachokipenda.

"Nikila chipsi nalala na naamka vizuri na ni muda mrefu utaratibu wangu ni huo. Sijawahi kupatwa na magonjwa ya aina yoyote tofauti na kuona ongezeko la mwili, ambao hauna madhara kwangu," anasema.

Mkazi wa Nyasaka, mkoani Mwanza, Rebeca Nkaila, anasema mazingira ya upatikanaji wa chakula hicho mahali pa kazi pamoja na gharama, ndiyo sababu inayomfanya yeye pamoja na wengine kukimbilia chipsi.

Naye Mkazi wa Majengo, wilayani Magu mkoani Mwanza, Khadija Idd, anasema chakula chake pendwa ni chipsi kwa sababu ni chakula rahisi cha haraka ambacho kinaweza kuliwa muda wowote bila kikwazo. Pia anasema maandalizi yake ya muda mfupi ni tofauti na kuanza kuandaa ugali au wali na mboga.

Mkazi wa Kijiji cha Ihayabuyaga, Magu mkoani Mwanza, Omary Kassim. anasema anatambua chakula hicho kuwa kina athari za kiafya ikiwamo uzito kupita kiasi, shinikizo la damu na magonjwa ya moyo, kutokana na mafuta mengi na chumvi zinazotumiwa kwenye maandalizi. Pamoja na kutambua athari za chakula hicho, anasema yote hayo wanamwachia Mungu.

Ni wazi kwamba ulaji wa chakula cha aina hiyo, una madhara kwa afya ya mtumiaji na wataalamu wa afya wamekuwa wakisisitiza watu kuchukua tahadhari.

Aidha, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2024, Godfrey Mnzava, hivi karibuni, aliwashirikisha ujumbe wa Mwenge akisema wananchi wazingatie utumiaji wa vyakula vyenye lishe bila kusahau matunda na mboga, ili kuboresha afya zao na kuacha kutumia vyakula ambavyo vinajaza tumbo.

### WAUZA CHIPSI WALONGA

Wafanyabiashara na watengenezaji wa chipsi, kutokana na chakula hicho kuchangamkiwa, wanasema wana uhakika wa kuuza wastani wa gunia moja na mafuta wastani wa lita 16 hadi 18 kwa siku, biashara ikiwa ya kawaida.

Mfanyabiashara katika eneo la Hamgembe mkoani Kagera, Godwin Elias, anasema kutokana na biashara hiyo kuonekana kupendwa, vijana wengi wameamua kuwekeza, hivyo kufanya idadi ya wauzaji kuwa kubwa na kuanza kugawana wateja.

Mfanyabiashara mwingine kutoka Malimbe jijini Mwanza, Emmanuel Kapesa, anasema wateja wengi wa chakula hicho ni wanawake kulinganisha na wanaume.

Anasema upatikanaji wa malighafi za chakula umerahisisha maandalizi ya chakula hicho na kukifanya kuwa chaguo la watu wengi, hasa wafanyabiashara ambao wana majukumu mengi na kukosa muda wa kuandaa chakula chenyewe.

### WATAALAM WAONYA

Ofisa lishe Mkoa wa Shinyanga, Yussuf Hamis, anasema kula chipsi si tatizo, bali tatizo ni matumizi ya muda mrefu hali inayozidisha kiwango cha vitu vinavyohitajika, ikiwa ni pamoja na kutokuzingatia mlo kamili.

"Si rahisi kubaini kama kuna madhara kwenye ulaji wa kupindukia wa vyakula vyenye mafuta mengi kupita kiasi kama chipsi. Lakini wanachotakiwa kutambua ni kuwa uandaaji wake hutumia mafuta mengi ambayo yakiingia mwilini pamoja na kiwango kikubwa cha wanga, husababisha magonjwa yasioambukiza yakiwamo kisukari, maradhi ya moyo, na shinikizo la damu," anasema.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki, magonjwa yasiyoambukiza yatokanayo na ulaji usiofaa, yamezidi kuongezeka kwa kasi, hivyo kuwa miongoni mwa magonjwa 10 tishio.

Dk. Msaki anasema magonjwa hayo ni pamoja na shinikizo la juu la damu, unaoshika nafasi ya kwanza kati ya magonjwa 10 yanayoongoza kwa watu wazima. Anasema katika hospitali hiyo, ugonjwa huo una wagonjwa 5,589 huku kisukari kikishika nafasi ya tano, kwa kuwa na wagonjwa 2,778.

Ofisa Lishe Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Abel Gyuga, anasema kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa magojwa yasiyoambukiza, kama shinikizo la juu la damu (BP), kisukari, vidonda vya tumbo, saratani na figo, kutokana na ulaji usiofaa na kuacha kula milo kamili kama inavyotakiwa.

Gyuga anasema takwimu za mwaka 2022 zinaonesha wagonjwa 2,372 wa nje waliokuwa wanaendelea kuchukua dawa kati ya hao, wagonjwa wa BP walikuwa wanaume 863 na wanawake 1,509; kisukari 671 wakiwamo wanaume 301 na wanawake 370.

Pia anasema waliolazwa katika hospitali ya wilaya kwa mwaka huo, 219 walikuwa na shinikizo la damu wanaume wakiwa 63 na wanawake 116, kisukari 26 kwa wanaume tisa na wanawake 17.

"Ukiangalia takwimu hizi wanawake wamekuwa waathirika wa maradhi haya na hii inatokana na mtindo wa maisha. Kwa sasa wakitumia kwa wingi vyakula vyenye mafuta ikiwamo chipsi na mambo mengine kama pombe kupita kiasi, sigara, kutofanya mazoezi na kutokula mlo kamili unaozingatia makundi matano ya lishe, yakiwamo mboga na matunda," anasema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Kisukari Tanzania (TDA), Prof. Andrew Swai, anasema magonjwa yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi na kuwaathiri watu wengi, wakiwamo watoto. Anabainisha kwamba vifo milioni 42 sawa na asilimia 71 duniani kote vilivyohusisha watu wa umri wa miaka 30-70 vilisababishwa na maradhi yasiyoambukiza.

"Mtu anaweza kuwa na magonjwa yasiyoambukiza kwa miaka kadhaa, bila dalili huku mwili ukiendelea kuathirika. Mfano shikizo la juu la damu, pia kisukari unaweza usiwe na dalili hadi macho, figo, moyo au mishipa ya damu au fahamu inapokuwa imeharibika vibaya, hivyo tunahitaji kubadili ulaji wetu," anasema.

Prof. Swai anasema kila mtu ahakikishe uzito unakuwa katika kiwango kinachofaa, kupunguza unywaji wa pombe na matumizi ya tumbaku.

Anasema matibabu ya magonjwa ya figo, moyo na kisukari ni ya gharama kubwa na yanatumia asilimia nne ya pato la taifa pia wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ambao wanasumbuliwa na maradhi hayo, wanatumia asilimia 20 ya mfuko.

- ***Imeandaliwa na Restuta Damian (KAGERA), Remmy Moka (MWANZA), Neema Emmanuel (MAGU), Vitus Audax (MWANZA), Alex Sayi (MASWA).***

## TFS kutumia setelaiti kudhibiti viashiria moto

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeanza kutumia teknolojia ya mifumo ya kufuatilia viashiria na matukio ya moto, kwa njia ya mtandao kupitia satelaiti.

Mifumo hiyo itawawezesha wahifadhi kuchukua hatua za haraka katika matukio hayo na kuyadhibiti, kwa kushirikina na wadau wengine .

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi wa TFS, Rodgers Nyinondi, alisema hayo juzi wakati wa mafunzo kwa wahifadhi kutoka Kanda ya Mashariki yaliyofanyika mkoani hapa.

Nyinondi ambaye ni mtaalamu wa ufuatiliaji na matukio ya moto msituni, alisema lengo la kujengewa uwezo huo ni wahifadhi kupata ujumbe wa matukio ya moto, kwenye maeneo wanayoyasimamia kupitia simu janja.

Alisema kuyapata kwa uharaka matukio hayo na kubaini viashiria vya moto, kutawarahisishia kudhibiti na kuyafikia matukio hayo kwa haraka zaidi na kuuzima.

Kwa mujibu wa Nyinondi, mafunzo hayo ni sehemu ya kwanza ya mpango wa muda mrefu, ambayo watapewa wahifadhi wote wa TFS nchini, ili kuwawezesha kukabiliana na matukio ya moto na kubaini viashiria vyake, kwenye maeneo yao. Hivyo kuchukua hatua za udhibiti.

" Hii ni sehemu ya kwanza ya mafunzo kutolewa na TFS kwa wahifadhi wa wilaya, mashamba ya miti na hifadhi ya msitu asilia wa Kanda ya Mashariki, lakini baadaye yataendelea maeneo mengine ya nchi," alisema. Nyinondi alisema lengo kubwa la mafunzo hayo ni kuhakikisha matukio ya moto yanadhibitiwa pale yanapotokea na pia katika kufuatilia viashiria vya moto, kabla hayajijatokea na kuchukua tahadhari.

Alisema mfumo huo wa kidigitali unatumia sateleiti zinazodhaminiwa na mashirika ya anga ya Marekani na nchi nyingine za Ulaya.

"Huu ni mfumo wenye kuleta tija, kwa haraka na pia ni mfumo rafiki. Kinachotakiwa ni kuwa na simu janja na kutumia mtandao na kungia na kuona matukio ya moto maeneo mbalimbali, ili kama uko jirani kuchukua tahadhari mapema," alisema.

Pia alisema teknolojia hiyo ilivyo, TFS itaendelea kuwafundisha wataalamu wake ambao nao watawafikia wananchi na kuwafundisha mifumo hiyo, ambayo itawasaidia watu kuchukua tahadhari ya baadaye.

Naye Ofisa Mhifadhi, Zarina Shaweji, kutoka Hifadhi ya Mazingira ya Asili Uluguru, alisema mafunzo waliyopata ya kutumia satelaiti kwa kutumia mtandao ya kutambua au kupata vashiria vya moto unaotokea msituni, yamekuwa ya muhimu.

Alisema njia hiyo inawezesha wahifadhi hata wanapokuwa nje ya misitu kutambua moto unaotokea ndani ya msitu, kwa kupata ujumbe katika simu.

Kaimu Kamanda wa TFS Kanda ya Mashariki, Matthew Ntilicha, aliwataka wananchi kuwa mabalozi katika masuala ya udhibiti wa moto katika misitu ya asili na hifadhi .

Ntilicha alisema TFS imeandaa programu ya kupita kwenye shule mbalimbali ndani ya kanda hiyo, ili kuzungumza wanafunzi baada ya kubaini nyakati za likizo wanafunzi kwa baadhi ya maeneo wanashiriki kwenye suala la moto bila ya wao kuwa na uelewa. Alisema program hiyo, itaanza kutekelezwa katika shule zilizoko kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi na itakuwa chachu kwa wanafunzi kushiriki mapambano dhidi ya moto na kuchangia kudhibiti viashiria vya moto, kwenye maeneo ya hifadhi.

# Majaliwa awaasa vijana mikopo kausha damu

**Na Vitus Audax, MWANZA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka vijana nchini kutojihusisha na mikopo yenye masharti magumu, maarufu kama 'kausha damu' kwa kuwa itawafanya waishi maisha magumu na hatimaye kushindwa kutimiza malengo yao.

Majaliwa alisema hayo juzi wakati akifungua Maonesho ya Wiki ya Vijana Kitaifa, yaliyofanyika jijini hapa, huku akisema haiwezekani taasisi kutoa mikopo kwa asilimia 100 na ikitakiwa kurejeshewa ndani ya muda mfupi.

Alisema ukopeshaji wa namna hiyo hautakiwi kufuatwa na vijana wala watu wa aina yoyote, kwa kuwa hakuna maendeleo bali ni maumivu kwa mkopaji.

"Nawasihi sana msiende kwenye mifuko ya ukopeshaji inaitwa kausha damu, wana mashari#ti magumu. Eti anakukopesha leo Ijumaa (juzi) anakwambia Ijumaa ijayo zote zirudi, halafu ukirudi anataka kama hiyo hiyo uliyoikopa. Hii haiwezekani.

"Asilimia 100 haiwezekani hata benki walitaka watoe asilimia 15 tuliwaambia ni ngumu kwa Watanzania. Hawa wananchi wa kawaida, sasa hivi wameshuka wako kwenye nane, saba, sita na tunaendelea ikiwezekana waende kwenye tano, nne hata moja," alisema Majaliwa.

Pia alisema katika kukabiliana na suala hilo, serikali imeweka utaratibu maalum wa kupata mikopo kwa masharti nafuu kupitia Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema katika program hiyo iliyoko chini ya Kurugenzi ya Uwezeshaji Kiuchumi, umefanyika uwekezaji wa miradi ya zaidi ya Sh. bilioni 1.6 inayowanufaisha zaidi ya wananchi milioni 3.7.

Waziri mkuu alisema wanufaika katika uwezeshaji huo, ni vikundi mbalimbali kwa kuelimishwa na kupata fedha zenye masharti nafuu na pia ipo mikopo ya halmashauri ya asilimia 10 iliyoanza kutolewa mwezi huu, baada ya kufungwa kwa muda, ili kupata njia sahihi ya utoaji huduma hiyo.

Pia alisema serikali inatambua juhudi na uwapo wa vijana na kuwataka kutobaki nyuma katika mabadiliko ya sayansi na teknolojia, bali waungane na wengine kwa kuwa yana mchango muhimu katika kusaidia kufanya uamuzi wenye tija katika shughuli mbalimbali.

"Kila mmoja ajikite kwenye eneo hili la teknolojia, ili turahisishe utendaji kazi nchini na sisi tunaendelea kunyoosha fursa za vijana, ili kila mmoja azione na kushiriki ipasavyo kujipatia mafao kwenye maisha yake," alisema.

Majaliwa pia alisema serikali inatambua na kuheshimu mchango wa vijana nchini na mikakati mbalimbali imeendelea kutekelezwa na taifa, ili kuhakikisha kila kijana anapata fursa kwa ajili ya maendeleo yake binafsi na taifa.

Kuhusu ajira, Majaliwa alisema Tanzania ni moja ya nchi zinazokabiliwa na tatizo hilo duniani na kwamba, juhudi mbalimbali zimeendelea kufanyika ikiwa ni kuzalisha ajira takribani 162,968, zikiwamo 112,572 katika ujenzi na 21,445 sekta ya madini.

"Tukisemea ajira watu wanawaza kupata kwenye ofisi za halmashauri, mkuu wa mkoa na wizarani na Tanzania nzima, tuna watumishi wasiozidi milioni mbili na nchi nzima tuko zaidi ya milioni 62.

Hiyo ni ngumu na si kwetu tu ni duniani kote na serikali inachokifanya ni kufungua milango ya ajira serikalini na sekta binafsi na zile shughuli mbalimbali za kujipatia pato binafsi," alisema.

Alisema kupitia programu iliyoanzishwa mwaka 2001 wanaratibu programu inayogharamiwa na serikali kwa miezi sita, ili kuwaimarisha vijana katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi kwa lengo la kuwapa ujuzi na wakitoka huko wajiajiri na kuwa na sifa za kuajiriwa.

Alisema wanaimarisha fursa za upatikanaji wa elimu kuanzia awali mpaka kidato cha sita bure na vyuo vikuu, ambako kuna utaratibu wa kuchangia.

Alisema mikopo hiyo imeendelea kupanda kutoka Sh. bilioni 400 hadi 700 na kwamba, serikali imeendelea kufungua milango ya ajira katika sekta mbalimbali za binafsi na serikalini kwa wazawa, ili vijana wapate fursa.



Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kulia), akibofya kitufe kuzindua Benki ya Access, iliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwisho mwa wiki. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Imani John; Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Saada Kassim Msem na Mwenyekiti wa Bodi BoT, Janet Lekashingo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vijana 1,400 wamuenzi Nyerere kutembea Mwitongo hadi Mwanza

**Na Timothy Itembe, MARA**

IKIWA kesho ni kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, vijana 1,436 kutoka mikoa yote Tanzania, wameanza matembezi kwa ajili ya kumuenzi kutoka kijiji alichozaliwa cha Mwitongo, Butiama mkoani Mara, hadi Mwanza.

Maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 25 ya Mwalimu Nyerere ambayo yataambatana na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, yatafanyika kesho jijini Mwanza na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluihu Hassan.

Matembezi hayo yamezinduliwa juzi na Makamu Mwenyekiti Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Rehema Sombi.

Sombi alisema matembezi hayo yanalenga kumuenzi Mwalimu Nyerere, Rais Awamu ya Kwanza na kuwataka vijana, jamii kuendelea kudumisha amani iliyoasisiwa na kiongozi huyo.

Alisema matembezi hayo yatachukua siku tano hadi hitimisho ya kilele cha siku ya kuzima mbio za Mwenge wa Uhuru, jijini Mwanza.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa Mara, Mary Daniel, aliwasisitiza vijana kuunda vikundi na kuchangamkia fedha za mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ya asilimia 10 ya makusanyo ya ndani katika halmashauri, kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alisema safari hiyo ya matembezi ni ya kihistoria kutokana maandalizi ya Nyerere, alipoanzia mchakato wa kutafuta Uhuru wa nchi na kujikwamua kutoka mikono ya utumwa wa wakoloni na harakati zilizaa matunda.

Prof. Muhongo alisema vijana walioshiriki matembezi ya mshikamano kwenye taifa kuanzia Mwitongo, alipoanzia matembezi ya kwanza mwaka 1967 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwenda Mwanza, wametia hamasa ya mfano wa kuigwa kwa wenye nia ya kufanya hivyo na ni moyo wa hali ya juu wa kizalendo.

Katibu Mkuu wa UVCCM, Jokete Mwegelo, alisisitiza kuwa matembezi hayo ni utekelezaji wa maazimio ya viongozi yaliyoazimiwa Agosti, mwaka huu, mkoani Iringa kuwa yafanyike kwa lengo la kumuenzi Baba wa Taifa na yaanzie alikoanzia matembezi mwaka 1967 kijijini Butiama.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kumuenzi Nyerere ni kuyaishi matendo na mambo aliyoyaamini

**WATANZANIA** wapenda haki na amani Afrika na duniani kote, kesho wataadhimisha Kumbukizi ya Miaka 25 ya kifo cha Rais wa Kwanza na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Maadhimisho ya mwaka huu, ambayo yanafanyika sambamba na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024, yanafanyika jijini Mwanza na mgeni rasmi atakuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Maadhimisho hayo, kama ambavyo yamekuwa yakifanyika kila mwaka, yalitanguliwa na midahalo na makongamano mbalimbali kujadili masuala anuai yakihusisha fikra, falsafa na mitazamo ambayo aliviishi na kuvitenda wakati wa uhai wake.

Miongoni mwa mambo hayo ni elimu, ukombozi wa Afrika, vita dhidi ya rushwa, utawala bora huku akisisitiza uadilifu kwa viongozi, kutojilimbikizia mali na vitendo vya rushwa.

Kwa ujumla, tangu alipofariki dunia, ni miaka 25 ambayo kwa baadhi ya vijana waliokuwa watoto na waliozaliwa wakati huo au miaka michache baadaye, kwa sasa ni wakubwa ama wameoa au kuolewa lakini fikra, matendo na falsafa zake bado vinaishi na pengine ni muhimu kuliko wakati ule.

Moja ya mambo hayo ni mapambano dhidi ya rushwa. Nyerere alikemea waziwazi vitendo vya rushwa, ikiwamo watu kutoa rushwa, ili kupata huduma au kutumia fedha kupata uongozi.

Alisema waziwazi kwamba mtu anayetumia fedha kupata uongozi, huyo hafai kwa sababu anafanya hivyo kwa manufaa binafsi badala ya wananchi wanaompa kura.

Kwa mantiki hiyo, alihimiza watu wanaotaka uongozi wajichunguze kuhusu usafi wao na maadili. Alisema fedha kisiwe kigezo cha mtu kupata uongozi bali uadilifu.

Jambo lingine alilolisisitiza ni elimu, huku akisisitiza kuwa iwe nguzo ya kumkomboa Mtanzania kifikra, ili kuyatawala mazingira yanayomzunguka, ikiwamo kutatua vikwazo vinavyomkabili yeye na jamii yake.

Kuhusu Muungano, alisisitiza kuwa unapaswa kulindwa kama mboni ya jicho na mtu yeyote atakayediriki kuuchezea, hana budi kushughulikiwa kwa gharama zozote.

Licha ya mambo hayo, Nyerere alikuwa akisisitiza Afrika kuungana na kuwa na nguvu moja, ili kujikomboa kiuchumi baada ya mataifa mengi kupata uhuru kutoka kwa wakoloni.

Katika uongozi wake viwanda vingi vilijengwa, huku akisisitiza matumizi ya bidhaa za ndani zinazotokana na viwanda hivyo. Alisisitiza pia watu kufanya kazi kwa bidii na kutaka wavivu, wazembe na wazururaji wachukuliwe hatua.

Wakati kesho atatimiza miaka 25 tangu alipofariki dunia, mambo aliyoyasisitiza na kuyapiga vita bado yanatendeka. Rushwa bado ipo katika maeneo mbalimbali, ikiwamo baadhi ya watu kutafuta uongozi kwa kutoa rushwa.

Ni vyema katika kumuenzi, Watanzania wakaziishi fikra na falsafa zake, kwa kufanya kazi kwa bidii kama alivyohimiza. Pia viongozi wanapaswa kujiepusha na vitendo vya rushwa na kutenda haki.

Wakati mwaka huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa, ni vyema Nyerere akaenziwa kwa watu wanaotafuta uongozi kwa rushwa, wakawekwa kando na wananchi kuchagua watu waadilifu. Pia vyama vya siasa katika hatua za mchujo, viwaondoe wale wote wanaoendekeza rushwa katika kusaka uongozi.

Kwa jumla, katika kumuenzi Nyerere, njia pekee ya kufanya hivyo ni kuyaishi matendo yake na kuheshimu fikra na falsafa zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tumuenzi Nyerere kwa kuimarisha uchumi wa viwanda

**KESHO** ni kilele cha kumbukumbu ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyefariki dunia Oktoba 14, mwaka 1999 nchini Uingereza.

Lakini kabla ya kuendelea, ninaomba nikumbushe kuwa, yeye ndiye ambaye kwa kutambua umuhimu wa rasilimali za Tanzania, alianzisha viwanda vingi, ili kujenga taifa imara linalojitegemea kiuchumi.

Alichukua hatua hiyo, kutokana na ukweli kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi, yakiwamo madini kama Tanzanite yanayopatikana Tanzania pekee.

Mbali na madini, Tanzania ina mbuga za wanyama, mlima Kilimanjaro, milima na mabonde, misitu, ardhi yenye rutuba, mito, maziwa na bahari, huku baadhi ya mazao ya rasilimali hizo yakisaidia katika shughuli za uzalishaji kwenye viwanda.

Viwanda vilijengwa, ili kuimarisha uchumi kwa kupata malighafi kutoka kwa wakulima na kutengeneza bidhaa kabla ya kuuza katika soko la ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya viwanda hivyo ni Mwatex, Mutex, Kilitex, Sungura Textile, Mbeya Textile, Urafiki Textile, Tanganyika Packers na UFI ambavyo vingi kwa sasa vimebaki kama magofu kwa kushindwa kuzalisha.

Vilevile kulikuwa na viwanda vya kutengeneza bidhaa za viwandani, viwanda vya kahawa Moshi na Bukoba, viwanda vya saruji Tanga, Dar es Salaam na Mbeya, kiwanda cha matairi Arusha, kiwanda cha sigara Dar es Salaam na vingine vingi.

Alichukua hatua hiyo kwa kuamini kuwa, ili Tanzania iweze kuendelea ni lazima kuwa na viwanda vya kutosha hasa viwanda vya umma, kwa kuwa uchumi wa viwanda utaliepusha taifa kuwa tegemezi.

Juhudi za mwanzo za Mwalimu Nyerere za kuweka mkakati wa kuendeleza viwanda, ilikuwa katika mpango wa kwanza wa miaka mitano mwaka 1964, huku ukitoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo.

Mpango huo ulilenga kuvutia wawekezaji wa ndani kuanzisha viwanda vitakavyozalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi, badala yake zipatikane Tanzania.

Ninadhani itakuwa ni vyema kama Baba wa Taifa ataenziwa kwa kufufua viwanda alivyoanzisha enzi wza utawala wake, ili kusaidia vijana wengi kupata ajira badala ya kuviacha vikiwa magofu.

Kwa mfano kiwanda cha nguo cha Urafiki, kwa muda mrefu majengo yake yamekuwa ni magofu hadi hivi karibuni kilipochukuliwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Baba wa Taifa alitamani Tanzania iwe nchi ya uchumi wa viwanda ndio maana alianzisha viwanda vingi, hivyo ndoto zake zingeendelezwa, ili kufikia kile ambacho alitamani kiwe kwa nchi hii changa.

Tanzania ilipitia hatua mbalimbali, ndipo mwaka 1974, serikali ilizindua mpango wa tatu wa miaka mitano, uliolenga kuongeza kasi ya mabadiliko ya kimuundo kwenye mwelekeo wa kujitegemea.

Juhudi za kuendeleza sekta ya viwanda, ililenga usindikaji wa mazao ya kilimo na kuzalisha bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi, 'viwanda msingi', kukuza uwezo wa Tanzania kujitegemea.

> **Tanzania ilipitia hatua mbalimbalik, ndipo mwaka 1974, serikali ilizindua mpango wa tatu wa miaka mitano uliolenga kuongeza kasi ya mabadiliko ya kimuundo kwenye mwelekeo wa kujitegemea.**

Kujitegemea kulikuwa katika uzalishaji wa viwanda pamoja na kutimiza mahitaji ya msingi ya maisha ya binadamu, kwa ajili ya Watanzania. Kwa ujumla ni kwamba, kujitegemea katika mazingira ya sekta ya viwanda ilikuwa ikitafsiriwa kuwa ni uhuru wa kiuchumi.

Hatua hizo za Mwalimu Nyerere, zililenga kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya taifa kiuchumi na kuwakwamua Watanzania kutoka katika umaskini uliokuwa unawakabili.

Tunapofikia kilele cha maadhimisho ya miaka 25 ya kifo chake, ni vyema tukamuenzi kwa kufufua viwanda alivyoanzisha enzi ya utawala wake, ili kuimarisha uchumi wa viwanda.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Utashi wa kisiasa unahitajika katika nishati safi ya kupikia



Pascal Mayalla

LEO naendelea na sehemu ya pili na ya mwisho ya nishati safi ya kupikia. Watanzania ni wazuri sana kwa mahubiri lakini inapokuja kwenye suala la kutekeleza kwa vitendo kile kinachohubiriwa ni mbingu na nchi.

Kwa sasa, kuna hii wimbo mpya ya Nishati Safi ya Kupikia, ambayo mhusika mkuu wake ni Rais Samia Suluhu Hassan na mkazo umewekwa kwenye gesi ya majumbani na matumizi ya nishati jadidifu.

Wiki iliyopita, niliishia kutoa wito wa hiki kinachofanywa na kampuni ya mafuta ya TotalEnergies, kuunga mkono juhudi za Rais Samia kwa kuanza kusambaza gesi ya kupikia kwenye vituo vyake zaidi ya 100, vilivyotapakaa nchini kote.

Niliishia kutoa sababu ya ni kwanini Watanzania wengi bado wanakumbatia matumizi ya kuni na mkaa kwa nishati ya kupikia? Nikajijibu kwamba jibu ni moja tu. Majiko ya gesi ni gharama na pia gesi ni gharama. Majiko ya umeme na gharama za umeme ni ghali kuliko mkaa na kuni. Mkaa na kuni kwa vijijini ni bure.

Ughali huu unachangiwa na kodi na tozo mbalimbali, hivyo kama serikali inataka suala hili lifanikiwe na Watanzania watumie gesi, na ina utashi wa kisiasa (political will), napendekeza yafuatayo;-

Pendekezo la kwanza na kuu ni uwepo wa utashi wa kisiasa wenye nia ya dhati ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ya gesi na umeme badala ya kuni na mkaa. Kwa vile kampeni hii inaongozwa na Rais Samia mwenyewe, tunaweza kusema utashi wa kisiasa upo, lakini je, kuna hatua zozote mahsusi za dhati kuhakikisha Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia?

Pili, serikali ifute kodi zote kwenye majiko ya gesi, mitungi ya gesi na gesi yenyewe na kwenye majiko ya umeme na kushusha gharama za umeme. Kuna ubaya gani serikali ya Mama Samia, ikaondoa kodi zote ikiwamo ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye majiko ya gesi, umeme na gesi ya kupikia? Mbona kwenye kompyuta tumeondoa kodi?.

Hawa Watanzania wenzetu 22,000 wanaofariki dunia kila mwaka kwa matatizo yanayosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa, maisha yao yangeokolewa kwa matumizi ya gesi na umeme.

Tatu, wanasheria tuna msemo wa “exhaust local remedies” yaani kabla hujatafuta msaada wa nje, anza na kile ulicho nacho. Waswahili wanasema fimbo ya mbali haiui nyoka bali ile uliyo nayo mkononi. Kwenye huu mkakati wa Rais Samia wa nishati safi ya kupikia, nishati ya gesi ni fimbo ya mbali inayohitaji mitungi na kusafirishwa.

Kwa sasa zaidi ya asilimia 90 ya nchi yetu, tuna umeme, hivyo fimbo ya kweli ya karibu ni majiko ya umeme na sasa kuna majiko banifu ya umeme mdogo kama vile ‘rice cooker’, ‘fryers’ na ‘pressure cookers’. Serikali iondoe kodi kwenye vifaa vya umeme wa kupikia. Kama kwenye kompyuta tumeweza, tunashindwa vipi kwenye majiko ya gesi na umeme?.

Nne, serikali itambulishe ruzuku ya majiko ya gesi, umeme na mitungi ya gesi, kama ilivyo kwa ruzuku kwenye zana za kilimo na pembejeo ikiwamo mbolea. Ni jambo la kufurahisha jambo hili limeshanza baada ya serikali kutoa ruzuku ya asilimia 50 kwa mitungi ya gesi inayosambazwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Enzi za uongozi wa awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere, baadhi ya bidhaa muhimu, zikiwamo mbegu, mbolea na pembejeo za kilimo, zilifanywa bei nafuu kuliko hata bei halisi kwa kupewa ruzuku ya serikali, ili wananchi wamudu gharama.

Kuna wakati wa uhaba wa maji, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa linatumia gharama kubwa kuzalisha umeme wa gesi na mafuta na kuuza kwa bei ndogo kama ya umeme wa maji, ili kutowabebesha wananchi mzigo mkubwa wa gharama. Kwa hiyo katika kutekeleza kampeni ya nishati safi ya kupikia, serikali inapaswa kufanya hivyo.

Tano, wafadhili mbalimbali wahamasishwe kujitolea kufadhili majiko na mitungi ya gesi kwa wasio na uwezo, wakiwamo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), waingize programu ya kufadhili majiko, mitungi na ruzuku ya gesi kwa kaya maskini katika mpango wao wa kunusuru kaya masikini.

Sita, mamlaka za serikali za mitaa, kwa maana ya halmashauri, zitunge sheria ndogo kulazimisha taasisi zote za watu wengi kama shule, vyuo vya kati, vyuo vikuu na hoteli ni lazima kutumia ama nishati itokanayo na kinyesi na mimea (biogas) au gesi, ili kuokoa mazingira na sheria za ujenzi zijumuishe njia za gesi kama ilivyo kwa mabomba ya maji, umeme na mawasiliano. Pia watu walipe bili za gesi kama maji na umeme. Saba, ziwekwe tozo maalum kwa vibali vya mkaa na ziwekwe faini kali kwa uharibifu wa misitu kutafuta kuni na uchomaji mkaa bila vibali. Kama TANESCO iliweza kuuza umeme kwa bei ya chini na enzi za Mwalimu kulitolewa ruzuku kwenye bidhaa muhimu na enzi za JPM gharama za kuunganishwa umeme wa REA zilikuwa Sh. 27,000 tu na tumeshuhudia hadi vijumba vya nyasi vimeunganishwa na umeme, hili linashindikana vipi kwenye gesi?

Nane, tuongeze matumizi ya mkaa wa mawe na mkaa mbadala na kuongeza matumizi ya majiko banifu. Tisa, wenzetu walioendelea, gesi inasambazwa majumbani kwa mabomba kama maji na umeme na vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba la gesi, visambaziwe gesi majumbani kama Ulaya,

Tulielezwa gesi itasambazwa hadi majumbani. Kama TANESCO wameweza kusambaza umeme kote, maji pia yamesambazwa kote, TTCL inasambaza mkongo wa taifa hadi majumbani, kunashindikana nini kusambaza gesi hadi majumbani watu wakalipa bili za gesi kama Ulaya?

***Mungu Mbariki Rais Samia***
***Mungu Ibariki Tanzania***
***Paskali***
***+255 754 270403***

# SUMAJKT kutekeleza miradi Comoro

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), limeingia makubaliano maalum na Kisiwa cha Ngazija cha Comoro, yanayolenga kufanya biashara mbalimbali na ujenzi wa barabarani kisiwani humo.

Utiaji saini wa makubaliano hayo ulifanyika jana, mkoani Dar es Salaam, kati ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele pamoja na Gavana wa Kisiwa cha Ngazidja, Mze Mohamed Ibrahim.



Gavana wa Kisiwa cha Ngazidja Comoro, Mze Mohamed Ibrahim (kushoto) na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa (SUMAJKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, wakitia saini hati ya makubaliano ya kufanya biashara kati ya SUMAJKT na kisiwa hicho, hafla iliyofanyika mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: Mpigapicha Wetu**

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, Meja Jenerali Mabele, alisema yanakwenda kufungua fursa kwao kwa kuhakikisha wanafanya biashara na kisiwa hicho, ili kuleta nchini fedha za kigeni.

“Ushirikiano kati ya Comoro na Tanzania ni wa kihistoria, wananchi wa nchi hizi mbili hasa visiwa vya Unguja, wamekuwa jamii zinazoshabihiana, hivyo tumekuwa na ushirikiano kabla ya uhuru.

“SUMAJKT katika kutafuta fursa za biashara tulikwenda visiwa vya Comoro na wenzetu wametukaribisha tufanye nao biashara. Wametukaribisha kufanya kazi katika biashara, mfano ujenzi wa barabara,” alisema.

Meja Jenerali Mabele, alisema kupitia makubaliano, SUMAJKT wanakuwa wakala wa Kisiwa cha Ngazidja kwa upande wa Tanzania, hivyo watasafirisha biashara mbalimbali, ikiwamo mifugo kama ng'ombe na mbuzi hai kwenda visiwani humo kama kitoweo.

“Kupitia makubaliano haya, pia tutafanya biashara ya mazao. Kwa sasa wametuambia wanahitaji mchele, tutafanya hizi biashara kwa pamoja. Yapo maeneo mengi zaidi ya ushirikiano,” alisema.

Meja Jenerali Mabele, alisema katika mazungumzo yao kisiwa hicho pia kimekaribisha SUMAJKT kufungua ofisi kisiwani humo, ili kuratibu shughuli mbalimbali watakazozifanya huko.

“Tumeanzisha ushirikiano huu na ndio maana tumeingia makubaliano haya, ili sisi tuwe karibu. Biashara ya Kisiwa cha Ngazidja, fursa zote walizonazo watatushirikisha SUMAJKT mahitaji yao na sisi tutahakikisha tunasaidia kupeleka kwa kuzingatia taratibu za nchi.

“Sehemu ambako kunahitaji kodi kulipwa italipwa, taratibu za nchi zitafuatwa kuhakikisha biashara hii inafanyika vizuri,” alisema.

Meja Jenerali Mabele, alisema wanapokwenda kufanya biashara kisiwani humo au kujenga barabara hawajengi tu, bali zitajengwa kwa faida, ili nchi kuingiza fedha za kigeni.

Alisema kupitia makubaliano hayo, SUMAJKT inaondoka katika kufanya biashara katika nchi moja na kwenda katika mataifa mengine, ili kuongeza fedha za kigeni nchini.

Gavana wa Kisiwa cha Ngazidja nchini Comoro, Ibrahim, alisema wamepata fursa ya kuonana na SUMAJKT, kwa lengo la kushirikiana katika maeneo tofauti.

“Biashara ya Comoro na Tanzania haijaanza leo imeanza zamani. Pia tunafanana katika mengi ukiangalia mila na lugha tunafanana, tumekuja kuendeleza ushirikiano ambao ulikuwapo.

“Ujio wetu umelenga kufanya biashara na kuziendeleza. Tukipata watu kama SUMAJKT, wafanyabiashara wetu watanunua vitu vyao na kuvikabidhi SUMAJKT na watafuatilia hadi vifike nyumbani,” alisema.

Ugeni huo ambao upo nchini tangu wiki iliyopita, mwanzoni mwa wiki ulipata fursa ya kujua shughuli zinazotekelezwa na SUMAJKT, kwa kutembelea kiwanda cha taa, matrekta, nguo na cha maji.

Dhima ya Shirika la SUMAJKT ni kuanzisha na kuendesha shughuli za uzalishaji mali na huduma kwa tija katika sekta za ujenzi, viwanda, kilimo, uvuvi na ufugaji na sekta ya biashara.

MAKALA

## SUMAIYA;

# Mwandishi aliyegeuka dereva magari ya kubebea makontena

- **Ni wa kwanza kuwa na leseni daraja C, mwanamke wa kwanza Zanzibar kufanya kazi hiyo**

**NA RAHMA SULEIMAN**

NI nadra sana Zanzibar kukutana na madereva wanawake wakiendesha magari makubwa ya kubeba mizigo (malori) ingawa sheria za nchi zinaruhusu. Lakini Sumaiya Ali Abdallah, 'ametoboa' na kuwa mwanamke pekee kwa Zanzibar, kuendesha gari hilo kama ni sehemu yake ya ajira ya kujipatia kipato.



Sumaiya, mwenye umri wa miaka 26, ni mmoja wa wanawake 300 wa Zanzibar wenye leseni ya udereva, lakini ni mwanamke pekee mwenye leseni ya daraja la C kwa magari makubwa ya mizigo.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, kuna madereva wenye leseni 10,717 kwa mwaka 2023 lakini kati ya hao, asilimia chini ya 10 ni wanawake.







Sumaiya, mtoto wa kwanza katika familia yenye watoto sita, huendesha lori la makontena na kituo chake kikuu cha kazi ni katika Bandari ya Malindi, Unguja. Hutoa mzigo bandarini hapo na kupeleka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya mji wa Unguja.

Hivi karibuni Nipashe ilimpata na kuzungumza naye, huku akibainisha kuwa tangu awali ni ndoto yake kuendesha magari makubwa baada ya kuona kazi hiyo ikifanywa zaidi na wanaume, wakati si haramu kwa mwanamke kuifanya.

"Kabla sijaanza kazi hii, nilikuwa natamani siku moja na mimi kuendesha magari makubwa ya kubeba mizigo, maana barabarani nikiwaona wanaume wakiendesha haya magari, nilikuwa nawaangalia na kujiuliza maswali hivi mimi siwezi kuendesha gari kama lile? Nashukuru kuwa hivi sasa maswali yangu yamepata majibu na kutimiza ndoto zangu," anasema.

Dereva huyo ambaye bado hajaolewa, anasimulia kuwa kazi ya kuendesha lori la mizigo bandarini hapo, amedumu nayo kwa miaka mitatu sasa na mwanzo alianza kuendesha gari la tani nne la kubeba mchanga na sasa anaendesha la tani 10.

"Mwanzo nilianza kuendesha gari la mizigo la tani nne, nikibeba mchanga eneo la Donge Kaskazini Unguja na kupeleka maeneo mbalimbali ya kisiwani hapa," anasema.

Wakati anaanza na kazi hiyo ya udereva wa magari ya mizigo, anasema baadhi ya watu walimshangaa na baadhi walimpongeza kutokana na ujasiri wake. Anasimulia kuwa waliokuwa wakimshangaa walitawaliwa na mfumo dume, ambao waliamini kuwa kazi hiyo ni ya wanaume.

Kwa sasa, anasema jamii inamuunga mkono kutokana na uamuzi wake huo na wakati mwingine anapokuwa barabarani ameshika usukani, hupokea pongezi nyingi kwa kupigiwa honi na madereva wengine, zikiashiria pongezi.

Anasimulia kuwa wakati mwingine akiwa barabarani anaendesha lori, hukutana na watoto wa kike na wa kiume wamejipanga barabarani, huku wakimpigia makofi na kumpongeza hasa nyakati watoto hao wakiwa wanarudi shuleni.

Sumaiya anasema kufanya kazi hiyo ya udereva hakumzuii kufanya majukumu mengine ya kifamilia kama mwanamke, ikiwamo usafi wa nyumba, kupika na kushiriki katika harakati zingine za kijamii.

**ALIACHA UANDISHI**

Anasema kabla ya kusomea udereva, alisomea fani ya uandishi wa habari ngazi ya stashahada na kuifanya kwa muda mfupi, lakini ilimshinda kwa sababu aliona bado hajatimiza ndoto yake.

Akizungumzia kuhusu rushwa ya ngono katika kazi hiyo, anasema hajakumbana na changamoto hiyo, kwa sababu anajiheshimu na anaheshimika kwa madereva wenzake kazini.

"Mimi ni mwanamke na bado sijaolewa. Wako ambao wananifuata kwa ajili ya kuanzisha uhusiano, haina maana kuwa labda ni ving'ang'anizi kutaka rushwa ya ngono. Unapowaambia ukweli kwamba siko tayari na hilo wanakuelewa", anasema.

CHANGAMOTO

Pamoja na kufanya kazi kwa ufanisi na kuipenda, anasema anakabiliana na changamoto, zikiwamo baadhi ya madereva hasa wa bodaboda kutofuata sheria za barabarani.

Sumaiya anawashauri wanawake wenzake kuacha kuchagua kazi kwa visingizio vya mitazamo hasi ya kwamba kazi ngumu ni za wanaume pekee.

Aidha, anasema hakuna aliyekuwa akijua kuwa Tanzania itaongozwa na Rais mwanamke, lakini imewezekana kwa Rais Samia Suluhu Hassan na anaendelea kuwaongoza wananchi vizuri, kama walivyokuwa wakiongoza watangulizi wake ambao wote walikuwa wanaume.

Sumaiya anaishauri serikali ya Zanzibar, kuongeza vyuo vya ufundi wa udereva wa magari makubwa ya kusafirisha mizigo kama ilivyo kwa nchi zingine, ikiwamo Tanzania Bara, ili ndoto za vijana wengi wa kike na kiume zitimie na kupata ajira.

"Udereva nilianza kujifunza hapa hapa Zanzibar lakini udereva wa malori ya kubeba mizigo nilijifunza chuo cha ufundi (VETA) Tanzania Bara, kwa sababu Zanzibar hakuna kozi hiyo," anasema

**FAMILIA YAKE**

Baba wa dereva huyo, Ali Abdallah, anasema amefurahi kumwona binti yake amechagua kazi anayoipenda mwenywe, ambayo inamwingizia kipato.

"Huu ni uamuzi wake mwenyewe na sisi familia yake na wazee wake kwa ujumla, tumeridhia na kumpa baraka zote binti yetu. Hii ni kazi kama kazi zingine", anasema.

Pia anasema ni vyema kuwaunga mkono watoto wenye vipaji kwa kuwaendeleza, ili kujipatia kipato halali ambacho kitasadia kuongoza familia zao.

**WANAHARAKATI KIJINSIA**

Wanaharakati wa haki za wanawake, wanasema kwa miaka mingi watoto wa kike walibaguliwa katika harakati za maendeleo kutokana na mifumo dume, iliyojengeka katika jamii.

Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, anasema mtoto wa kike akionekana ni mtu wa kulea familia na hastahili kufanya kazi ya kumuingizia kipato.

"Ndiyo maana uchumi wa wanawake ni mdogo ikilinganishwa na wanaume, kwa sababu tokea zamani mwanamke hakujengwa kuwa kiongozi, bali alijengwa kuwa ni mama wa kulea familia", anasema Dk Mzuri.

Aidha, anasema wakati umefika sasa kwa watu wa jinsi zote, kushiriki katika kila harakati za kimaendeleo, kiuchimi kisiasa na kijamii bila vikwazo.

"Unapomjenga na kumwandaa vizuri mtoto wa kike na wa kiume, unajenga jamii imara ambayo itakuwa haina ubaguzi wa kijinsia," anasema.

Sajenti Ali Abdallah, kutoka ofisi ya usalama barabarani makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, anasema madereva wanawake ni wazuri zaidi katika kufuata sheria za barabarani wanapoendesha vyombo vya moto, kuliko madereva wanaume.

Anasema katika ajali zinazotokea barabarani, nyingi husababishwa na madereva wanaume, kwa sababu mbalimbali ikiwamo uzembe wa madereva hao na kutofuata sheria za barabarani.

"Madereva wanawake huwa makini sana wanapoendesha magari na si rahisi kumkuta dereva mwanamke akiwa anaendesha gari kwa na makosa ya usalama barabarani. Laiti nchi hii ingekuwa na madereva wanawake watupu, ajali za barabarani zingekuwa chache mno," anasema.

Tangu Zanzibar kupata uhuru wake, sheria zake hazikumnyima fursa mwanamke kutoendesha gari kama ilivyo kwa baadhi ya nchi zingine, kwa mfano nchini Oman ambayo sasa imeondosha vikwazo hivyo.

Uzoefu wa nchi zingine, mfano Kenya, kwa mujibu wa Chama cha Madereva wa Malori nchini humo, kuna wanawake 100 wanaoendesha magari hayo makubwa hasa malori.

# MAISHA

OKTOBA 13, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 13

**Nguo nyeupe balaa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Jenga dari bora usije kujilaumu baadaye



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Madhara ya kujichubua

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | D | U | N | D | A |
| | U | | | E | |
| U | M | A | | R | |
| | A | | B | E | I |
| | Z | | | V | |
| W | A | N | G | A | |

## FUMBO TOTO





Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
CHA, IBA, TANGA, ASALI, ACHIKA, LIMBUA

## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI






## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akicheza na wenzake upenuni mwa nyumba yao, mara alikatiza paka akiwa amemkamata panya mdomoni mwake.

Juma alionekana kushangaa tukio hilo na kumuuliza mwenzake.

**Juma:** Itakuwaje panya kakamatwa kirahisi kama vile?

**Tom:** Paka ana nguvu na akili nyingi anamkamata panya kwa haraka.

**Juma:** Basi atakuwa sio mjanja kama yule panya Jerry katika televisheni.

**Tom:** Ile ni katuni tu, lakini panya sio mjanja kuliko paka

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ijue siri ya kufanikiwa katika maisha

***KARIBU** tena msomaji wangu tuendelee kuchambua maisha yetu yalivyo. Maisha ni fumbo na ukilifumbua unafanikiwa kirahisi sana.*

Katika maisha kuna ngazi tatu; mwanzo, katikati na mwisho na siku zote, mafanikio lazima uanze. Anza pale ulipo na kile kile ulicho nacho.

Kumbuka kuna imani ya kuanza na pia nguvu ya kuanza. Wako walioanza na hawajawahi kufika katikati. Neno la Mungu linauliza: "Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kumalizia?

"Asije akashindwa kuumalizia baada ya kupiga msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki wakisema, mtu huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu za kumalizia (Luka 14:28-29).

Watu wengi wanaanza lakini wanashindwa kumalizia jambo fulani. Matokeo yake anaishi kwenye uchungu na huzuni akijiuliza nini kimetokea?

Bila shaka imewahi kukutokea wewe kwamba mtu anakuahidi kitu, unapofuatilia anaanza kubadilika dakika za mwisho anaifuta ile ahadi. Kila siku hufikii malengo. Siku zote jifunze kumshirikisha Mungu katika mipango yako ya maendeleo. Muombe Mungu akupe nguvu ya kuanza na kumalizia jambo. Pia ombea waliokuahidi kwamba ahadi zao zitimie, wasijitoe, wasighairi!

> **Usiogope kujaribu tena na tena. Watu wengi leo hawafanikiwi kwa sababu huogopa kujaribu. Kama hujawahi kujaribu hutaweza kuja kushinda siku za usoni.**

Pia hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya. Zipo roho zinazoshambulia wale wanaokusaidia. Kwa mantiki hiyo, siku zote ombea sana wanaokusaidia katika maisha. Kuna wakati unakaribia kufikia malengo yako, halafu kitu kibaya kinatokea. Mtu yeyote aliyepanga na kufikia malengo, iko siri nyuma yake. Omba Mungu akupe nguvu ya kumalizia kwani mara nyingi matatizo yanatokea pale unapokaribia upenyo.

Na kwa wale wanaosaidia wengine, ni muhimu kwanza kutafuta historia yao. Hii ni kwa sababu unaweza kumsaidia mtu, kisha wewe ukafilisika! Wengine wana nuksi, maroho ya ukoo. Kama mtu aliwahi kumuua baba yake na wewe hujui ukamsaidia, Mungu atakuchapa na wewe.

Kingine wengi hawana maarifa. Huwezi kufanikiwa kama huna maarifa. Hakuna kitu kibaya kama kuishi gizani. Kwenye mafanikio hakuna bahati, ni siri. Kama hujafanikiwa jiulize maswali.

Shauku ni moja ya misingi ya mafanikio. Mungu hawezi kukupa kitu ambacho hujawahi kukitamani. Kifo cha mtu huanzia moyoni, iwe ni ndoa au biashara. Kila kitu huanzia moyoni, kwenye nafsi ya mtu. "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima". (Mithali 3:23).

Ukitaka uwe mtu wa shuhuda, nafsi yako iwe na shauku. Neno la Mungu linasema, heri waliao sasa maana baadaye watacheka. Shauku kubwa unayoanza nayo ndiyo itakayotoa mwelekeo utakuwa nani baadaye. Kiwango cha shauku ndiyo itaamua utafika wapi. Siri ya kupokea karama ya Roho Mtakatifu ni shauku. Usijikatae kwani hata wewe unaweza kufanikiwa. Wengi leo wanajibeza wenyewe na kusahau kwamba watu wengi waliofanikiwa ni watu wa kawaida kabisa.

Na mwanzilishi wa uongo ni shetani. Akiwadanganya watu kwamba eti kwa kuwa huna elimu huwezi kufanikiwa. Ukishaokolewa toka kwenye dhambi lazima uifahamu kweli ndipo utoke hapo uliopo!

Msomaji wangu, ili sasa ufanikiwe zingatia yafuatayo;- kwanza amini mwanzo mdogo. "Tena ujapokuwa huo mwanzo wako ulikuwa mdogo, lakini mwisho wako ungeongezeka sana"(Ayubu 8:7).

"Yeye ni mwenye hekima moyoni, na mwenye uwezo katika nguvu; Ni nani aliyejifanya mgumu juu yake, naye akafanikiwa? (Ayubu 9:4). Usipoamini mwanzo mdogo hayo makubwa unayotamani hutayafikia.

Kanuni ya kiroho ya mafanikio inatutaka tuanze katika mwanzo mdogo, lakini mwisho wake utaongezeka sana. Unachotakiwa kufanya ni kuondoa dhana ya kudharau mwanzo mdogo kwani huo ndio msingi wa mambo makubwa!

Usiogope kujaribu tena na tena. Watu wengi leo hawafanikiwi kwa sababu huogopa kujaribu. Kama hujawahi kujaribu hutaweza kuja kushinda siku za usoni. Waliofanikiwa walijaribu wakashindwa lakini hawakukata tamaa wakaendelea kujaribu tena na tena hadi kikaeleweka. Usiwe mtu wa kukata tamaa kirahisi, ng'ang'ania, komaa hadi kieleweke.

Tambua ya kuwa kushindwa kwako kumepangwa na kuzimu, lakini kushinda kwako kumepangwa na mbingu. Mbingu inataka uwe bilionea hivyo usikubali kubakia eneo la kushindwa!

Bakia kwenye kitu kile kile, usijaribu mara moja kuacha kwa kuwa hakijafanikiwa, ng'ang'ania pale pale, utaona mabadiliko. Ili ufanikiwe endelea kumtaabisha mtu akusaidie. Waliofanikiwa ni wale ving'ang'anizi.

***Niishie hapa, naamini umejifunza kitu. Je, una maoni? Ujumbe mfupi 0715268581. Namba ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Rais Samia amebadili 'fasta' maisha ya Watanzania

IDADI ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia imekuwa ikiongezeka kwa kiwango kidogo kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi asilimia 6.9 mwaka 2021.

Kwa matumizi ya kupikia, inakadiriwa kuwa takribani asilimia 90 ya kaya nchini, hutumia nishati ya kuni na mkaa kama nishati kuu ya kupikia. Hali hiyo inadhihirishwa na matumizi ya kuni, ambayo ni asilimia 63.5 na mkaa, ni asilimia 26.2

Asilimia 10 zilizobaki zinajumuisha asilimia 5.1 za LPG, asilimia tatu za umeme na asilimia 2.2 za nishati zingine.

Mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, unatokana na hitaji la kuwa na mpango jumuishi wa kitaifa katika kukabiliana na ongezeko la uharibifu wa mazingira na athari za kiafya, kiuchumi na kijamii zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia, kwa maana ya kuni na mkaa.

Novemba, 2022 Rais Samia Suluhu Hassan, alielekeza uandaliwe Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia, utakaotoa mwelekeo wa namna ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Aidha, Rais alielekeza kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wawe wamehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ndani ya kipindi cha miaka 10.

Kwa mantiki hiyo, madhumuni ya mkakati huo ni kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, salama, nafuu, endelevu na ya uhakika ya kupikia.

Mkakati huo umeainisha mikakati ya utekelezaji, shabaha, viashiria vya matokeo pamoja na wadau watakaokuwa na wajibu wa utekelezaji wa mkakati huu na majukumu yao. Masuala mengine yaliyoainishwa katika Mkakati ni muda wa utekelezaji pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wake

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia (WB) mwaka 2023, idadi ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia imekuwa ikiongezeka kwa kiwango kidogo kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 6.9 mwaka 2021. Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha wastani cha dunia cha asilimia 71 kwa mwaka 2021.

Kwa namna hali ilivyo sasa, nishati na teknolojia zinazotambulika kuwa safi kwa matumizi kutokana na kuwa na kiwango kidogo cha sumu, ni umeme, bayogesi, gesi asilia, LPG (Liquified Petroleum Gas), baioethano, nishati ya jua, majiko banifu na mkaa mbadala, wenye viwango vilivyothibitishwa na mamlaka ya kudhibiti viwango.

Tujifunze kwa wenzetu kama Kenya, ambao kanzidata ya WB, inaonesha mwaka 2023, asilimia 23.9 ya wananchi wake walikuwa wanatumia nishati safi ya kupikia.

Nchini Uganda, takwimu za WB mwaka 2023 zinaonesha asilimia 0.7 ya wananchi wake, walikuwa wanatumia nishati safi ya kupikia mwaka 2021.

Mathalani kwa Tanzania pekee, utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi wa mwaka 2017/18, matumizi ya nishati ya kuni yamekithiri hasa maeneo ya vijijini, ambako asilimia 84.8 ya kaya hutumia nishati hiyo, ikilinganishwa na maeneo ya mijini matumizi ni asilimia 17.4

Kwa mujibu wa Cooking Energy Action Plan ya Mwaka 2022, inakadiriwa takribani kiasi cha tani 10 hadi 12 za magogo huchomwa, ili kuzalisha tani moja ya mkaa.

Mkaa ni chanzo kikubwa zaidi cha nishati katika maeneo ya mijini, kwa kuwa unaaminika kuwa ni nafuu na hupatikana kwa viwango vidogo kulingana na kipato cha mtumiaji.

Vilevile, mkaa unasafirishwa, unasambazwa na kuhifadhiwa kwa urahisi. Kwa mujibu wa ripoti ya The Potential and Optimal Strategies for Charcoal Sub-Sector Development in Tanzania Mwaka 2019, matumizi ya mkaa yamekithiri maeneo ya mjini na zaidi ya asilimia 50 ya mkaa unaozalishwa nchini, hutumika Dar es Salaam.

Tanzania imekuwa ikiagiza LPG kutoka nje ya nchi, kwa kuwa utafutaji unaoendelea nchini bado haujagundua mafuta na hakuna kiwanda cha kuchakata mafuta ghafi.

Vilevile, gesi asilia iliyogunduliwa nchini ina kiwango kidogo cha propani (asilimia 0.3) na buteni (asilimia 0.06) ambacho hakitoshi kuzalisha LPG.

LPG iliyoingizwa nchini kwa mwaka 2022 ni tani za mraba 250,200 na kati ya hizo, tani za mraba 160,610 zilitumika nchini na 89,590 zilipita kupelekwa nchi jirani.

Aidha, matumizi ya LPG yameongezeka nchini kutoka tani za mraba 20,000 mwaka 2010 hadi 160,610 mwaka 2022.

Hakika! hakuna anayeweza kubisha kwamba Rais Samia, ameyabadili maisha ya Watanzania 'fasta' kupitia nishati safi ya kupikia.

***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI









Mwonekano wa harusi mbalimbali.

# MITINDO

## Nguo nyeupe balaa

MAVAZI yenye rangi nyeupe, hutafsiriwa kama nguo zenye heshima, mahaba na umaridadi.

Mara nyingi mwanamke akivaa vazi jeupe huonekana kwa haraka ni mtu mstaarabu, msafi na mwenye mahaba mazito.

Wadau wa mitindo wanaeleza kwamba nguo nyeupe ni nzuri kutoka nazo nyakati za jioni au usiku, wakati wa matukio maalum, kama harusi, kuvishana pete au kukutana na mpenzi wako kwa mara ya kwanza.

Kwa ujumla, aina hii ya mavazi ni sawa na upendo uliotukuka ulioko kwenye mwili.

Mavazi ya usiku ya pamba nyeupe 'Stephanie' huonesha haiba ya nchi na mapenzi.

Nguo zenye rangi nyeupe pia unaweza kuchanganya na rangi zingine, ili kunogesha zaidi kama dhahabu, nyekundu, nyeusi, bluu na zambarau.







## UREMBO

Na Mary Geofrey



# Madhara ya kujichubua

KATIKA baadhi ya sehemu duniani watu wanaamini kuwa ngozi ang'avu huashiria uzuri, utajiri na uwezo wa kifedha.

Katika baadhi ya sehemu watu wenye ngozi nyeusi huchukuliwa kuwa wapo chini ya kiwango, hii husababisha watu kutumia ving´arisha ngozi, kama krimu, vidonge au nyenzo zingine kubadilisha ngozi zao.

Tafiti zinaonesha kwamba wavulana na wasichana hupendelea kutumia bidhaa zinazong´arisha ngozi, ili kupata hadhi nzuri katika kundi la familia zao na jamii.

Mambo hayo yote huwa na athari kubwa juu ya mawazo ya vijana wa kiume na wakike, ambayo husababisha wachague chochote wanachomudu kati ya krimu au vidonge.

**MADHARA YA KUJICHUBUA**

Mtu anaeyejichubua anaweza kupata saratani ya ngozi, chunusi, uvimbe katika ngozi, ngozi kuwa nyembamba na kuongezeka kwa hamu ya kula.

Madhara mengine ni kuongezeka kwa uzito, kutokwa na mabaka, pumu ya ngozi, kupata watoto wenye kasoro na kupata matatizo ya akili.

Wataalam wa afya pia wanasema unaweza kuharibu ini, kuharibika kwa mishipa ya fahamu pamoja na figo kutokana na kiwango kikubwa cha zebaki zilizoko kwenye krimu.

Baadhi ya madhara haya huonekana mara moja na mengine hujitokeza kadri mtu anavyotumia ving´arisha ngozi.

## MAPISHI

# Nyama ya ng'ombe na njegere

MARA nyingi kwenye familia za Watanzania imezoeleka mapishi ya nyama ya rosti, unaweka viazi au nyanya chungu na bamia.

Mapishi ya nyama kwa aina ya mchuzi au rosti pia unaweza kupika kwa kuweka njegere na ukapata furaha.







**Mahitaji**

Nyama ya ng'ombe gramu 300, karoti moja, njegere gramu 150, vipande vya vitunguu maji, tangawizi na vitunguu saumu kila kijiko kimoja, chumvi kijiko kimoja, mchuzi wa sosi vijiko viwili, sukari vijiko viwili, siki vijiko viwili, maji ya wanga vijiko vitano.

**Namna ya kupika**

Osha nyama ya ng'ombe, halafu uikate iwe vipande vidogo vidogo, ondoa maganda ya karoti halafu uikate iwe vipande vidogo.

Washa moto, tia mafuta kwenye sufuria, mpaka yawe na joto la nyuzi 60, tia njegere, kaanga, halafu ziepue.

Washa moto tena, tia vipande vya vitunguu maji, tangawizi na vitunguu saumu kwenye sufuria koroga, tia vipande vya nyama ya ng'ombe, koroga halafu tia vipande vya karoti na koroga tena.

Weka tena sukari, siki, mchuzi wa sosi, chumvi, koroga, mimina maji ya wanga, koroga tia njegere koroga kisha uepue na upakue tayari kwa kuliwa na wali, ugali au tambi.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## Pambo la ukili, batiki kwenye nyumba

MVUTO wa chumba au sebule unaweza kuletwa kwa mapambo ya kienyeji rahisi, nafuu na kuonekana cha kisasa sana.

Baadhi ya mapambo haya ni yanayotengenezwa kwa malighafi za asili kutoka kwenye eneo ulipo na ukaleta upekee wa nyumba.

Wataalam wa mapambo ya ndani wanaeleza kwamba mapambo ya ndani ya asili yanaleta lugha ya tofauti ndani ya nyumba na mawasiliano mazuri kwa wageni.

Jambo la kuzingatiwa katika mapambo ya asili, kwa mujibu wa wataalam ni kuweka picha sehemu ambayo 'macho' yanapita kwa urahisi.

Miongoni mwa mapambo ya asili yanayotajwa na wataalam hao ni visahani vilivyofumwa kwa nyuzi nene zilizopangiliwa rangi au ukili ulionakshiwa kwa rangi.

Wanaeleza kuwa batiki iliyopangiliwa vizuri inaweza pia kutumika kuleta nakshi maridhawa ya asili.

Wataalam hao wanaeleza kuwa ukuta unaopanga kuweka pambo lako la asili unapaswa kuuandaa uonekane kama eneo la maonyesho ya kazi za sanaa.

Kitu kingine cha kuzingatia ni mpangilio wa mapambo kulingana na rangi. Inashauriwa kuweka rangi ang'avu au zilizopoa zinazoelekeana.

Wanaeleza kuwa pambo la asili ni rafiki wa mazingira kwa kwa kuwa linatumia malighafi rahisi zilizopo eneo husika.

Wataalam wanaeleza kuwa mapambo ya asili yanaweza kutengenezwa kwa miundo, tofauti mingi na kamwe hayachuji wala kupungua thamani.

Wanafafanua zaidi kwamba mapambo ya asili ya sanaa za nguo na ukili yametumika karne nyingi na 'fasheni' isiyoisha mvuto ambayo yanapatikana kwa gharama nzuri.





# Jenga dari bora usije kujilaumu baadaye

KATIKA nyumba leo, tunazungumzia umuhimu wa kuzingatia umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba.

Hii ni sehemu ambayo watu wengi wanaojenga nyumba husahau kuipa kipaumbele, lakini msanifu wa nyumba, Kimboi Mariki, anasema hiyo ni sehemu muhimu zaidi kwa sababu ndiyo hupendezesha zaidi nyumba.

Mariki anasema dari katika ujenzi wa nyumba mara nyingi watu wengi hawaipi umuhimu mkubwa lakini ni sehemu ambayo endapo haijamaliziwa vizuri, inaweza kuharibu kabisa kazi yote nzuri ya ujenzi wa nyumba iliyofanyika.

Pia anasema kwa sababu inaficha vitu vingi kwa ndani, endapo isipojengwa au kumaliziwa vizuri kitalaam inaweza kuleta athari kubwa kwenye nyumba.

"Dari imekuwa sehemu ambayo inasahaulika sana katika ujenzi wa nyumba zetu, kwa maana ya kuwa inapewa uangalizi kidogo sana. Lakini umaliziaji mzuri wa dari hili ndio unaozidisha uzuri wa nyumba yako. Inasaidia kuiweka imara na kwa usalama zaidi,"anasema.

"Dari ndiyo inaficha mabomba ya umeme na huduma zingine, ikiwamo kuondoa udhia kwenye macho ya watu wanaoingia au kuishi kwenye nyumba husika na kuipa mwonekano mzuri. Ili upate faida zote za dari ni vyema kumpata fundi au msanifu mzuri wa majengo anayeweza kusimamia kazi hiyo kwa ufanisi unaotakiwa," anasisitiza.


Anasema kabla ya kufanya uamuzi wa umaliziaji wa nyumba yako, ni vyema kujitafakari na kufanya uamuzi kwanza wa aina ya mwonekano wa dari unayoitaka kwenye nyumba yako, ili kuepuka kujilaumu baadaye.

"Tafakari na uamue, unataka kupata mwonekano gani, fanya uamuzi sahihi ni muundo gani wa dari unalolihitaji, usikurupuke, ukajilaumu baadae kumbuka kuna dari linalotakiwa kutengenezwa sebuleni, vyumbani, jikoni na hata vyooni. Na katika kila maeneo yote hayo unatakiwa kuamua.

"Unaweza kuamua mwonekano wa dari la sebuleni ukawa tofauti na wa vyumbani au ukafanana, hiyo yote itategemea na namna unavyopendelea wewe, lakini la muhimu kuzingatia ni kwamba unatakiwa kuhakikisha unatumia watu ambao ni wataalamu, ili walimalizie vizuri na kuiweka nyumba katika hali ya usalama zaidi," anasisitiza.






KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
NILIYETEMBEA NA MKEWE KAONEKANA ANAPANDA BASI LA MKOA ANAELEKEA 'SUMBAWANGA' MSAADA JAMANI!!!
INAMAANA TOKA NILIPOINGIA MADARAKANI HUYAONI MATOKEO?
NAYAONA SASA HIVI UNAITWA 'BONGE!'
NIMEKULA NAULI LAKINI HUU MWILI WA KIBUNGE NAONA AIBU HATA KUJIELEZA KWA KONDAKTA ANIBEBE BURE!
KITUO
MAPENZI YETU TULIKUTANA ULEVINI SIJUI IMEKUWAJE MPAKA UME-AMUA KUNIOA!
HURUMA USIENDELEE KUITWA 'JAMVI' LA WALEVI
ETI NINI BABA MWENYE NYUMBA?
UNATEMBEA NA ROHO YANGU NAKUOMBA SASA UIPUMZISHE UKAE ULE KODI... HATA MIMI NTALIPA
MBONA MIMACHO KODO KWANGU WAKATI MIMI MWENYEWE NN BUKU!
POMBE KILABU

## HABARI KIMATAIFA

# Mataifa duniani yashutumu Israel kushambulia walinda amani

**NEWYORK, Marekani**

MATAIFA mbalimbali duniani yamekosoa hatua ya jeshi la Israel, kushambulia Kituo cha Kikosi cha Walinda Amani cha Umoja wa Mataifa Lebanon (UNIFIL).

Wanajeshi wa Israel, walikishambulia kwa risasi jana, kituo kikuu cha uchunguzi UNIFIL kilichoko katika mji wa Naqoura, kusini mwa Lebanon na kuwajeruhi watu wawili.

Taarifa ya shambulizi hilo zilitolewa na Umoja wa Mataifa (UN), ikieleza vikosi vya Israel viliingia kinyume cha sheria, kwenye eneo jingine linalosimamiwa na UNIFIL, ambalo lilishambuliwa pia juzi Alhamisi.

China kupitia Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Mao Ning, ilisema ina wasiwasi na tukio hilo na kulaani vikali mashambulizi ya Israel, dhidi ya ujumbe wa amani wa UN.

Uturuki pia ililaani mashambulizi hayo yanayowalenga walinda amani na kusisitiza kuwa serikali mjini Ankara, itaendelea kuunga mkono operesheni kama hizo za kulinda amani.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari pembezoni mwa mkutano wa kilele wa Jumuiya ya Mataifa ya Kusini Mashariki mwa Asia (ASEAN), Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, alitoa wito wa kuchukuliwa hatua madhubuti, ili kuepusha vita kamili nchini Lebanon.

Alisema kuwa kuongezeka kwa migogoro katika eneo la Mashariki ya Kati, ni tishio kwa usalama wa dunia.

Aidha, Guterres alilaani pia mashambulizi ya Israel dhidi ya kituo cha UN na kuongeza kuwa askari wa kulinda amani lazima walindwe

"Amani inahitajika zaidi sasa kuliko hapo awali, unaposhuhudia mateso makubwa ya watu wa Gaza, ambayo sasa yameenea hadi nchini Lebanon, bila kusahau Ukraine, Sudan, Myanmar na kwengineko.

Nathubutu kuwaambia kwamba kiwango cha vifo na uharibifu huko Gaza ni mambo ambayo hayawezi kulinganishwa na hali nyingine yoyote ambayo nimeishuhudia tangu niwe Katibu Mkuu wa UN."

Huku hayo yakiarifiwa, watu 22 wameuawa na wengine zaidi ya 100 wamejeruhiwa mjini Beirut kufuatia mashambulizi ya Israel, huku chanzo kilicho karibu na kundi la Hezbollah kikisema kuwa mashambulizi hayo yalikuwa yakimlenga mkuu wa usalama wa kundi hilo Wafiq Safa.

Kwa upande mwingine Iran ilisema haitasita kuchukua hatua kali zaidi ikiwa Israel italipiza kisasi mashambulizi yake ya makombora ya hivi karibuni.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Araqchi, alisema jana kuwa serikali imejiandaa kikamilifu kukabiliana na uchokozi wowote.

Kauli hiyo imetolewa baada ya Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, kusema kuwa Israel itaishambulia Iran kwa njia sahihi ya kushangaza na itakayosababisha vifo.

**DW**



Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis (kushoto) akizungumza na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky (kulia), makao ya kanisa hilo mjini Vatican, juzi. **PICHA: AFP**

# Uchaguzi Msumbiji walalamikiwa

**MAPUTO, Msumbiji**

WAANGALIZI wa kimataifa kwenye uchaguzi mkuu wa Msumbiji, wameelezea kuwapo kwa matukio kadhaa ya udanganyifu wakati wa upigaji na kuhesabu kura.

Hata hivyo, vyama vya upinzani vimetoa kauli ya kupinga matokeo vikisema uchaguzi huo wa uliofanyika Jumatano, ulijaa wizi.

Katika taarifa yao ya hapo jana, waangalizi wa Umoja wa Ulaya walisema walishuhudia mabunda ya karatasi za kura zikiwa zimeshapigwa kwenye maeneo 10 tofauti.

Wasiwasi wa udanganyifu ulielezwa pia na Taasisi ya IRI ya Marekani, ambayo waangalizi wake walikosoa jinsi uchaguzi huo ulivyofanyika.

Kwa mujibu wa waangalizi hao, chama tawala cha Frelimo, kilitumia vibaya rasilimali za nchi, wakiwamo wafanyakazi na vyombo vya usafiri vya umma, wakati wa kampeni. Kwenye majimbo yenye wafuasi wengi wa chama hicho, usajili wa wapigakura ulivuka asilimia 100.

Waangalizi kutoka Jumuiya ya Madola, walitaka mamlaka husika kuyashughulikia madai yote ya udanganyifu.

Ingawa matokeo rasmi hayatazamiwi kupatikana kabla ya wiki mbili zijazo, mgombea wa Frelimo, Daniel Chapo, anatarajiwa kushinda kwa wingi wa kura.

**DW**

## Russia, Iran zakubaliana kuimarisha uhusiano

**TEHRAN, Iran**

MARAIS Vladimir Putin wa Russia na Masoud Pezekshian wa Iran, wamefanya mazungumzo na kuahidi nchi zao kuimarisha uhusiano wa kiuchumi.

Mkutano huo ulifanyika nchini Turkemistan juzi, viongozi hao walisifia kuimarika kwa uhusiano kiuchumi kwa mataifa yao na mitazamo yao inayofanana kwenye siasa za dunia.

Putin, ambaye nchi yake itakuwa mwenyeji wa mkutano wa kilele wa mataifa ya BRICS mjini Kazan, Oktoba 22 hadi 24 mwaka huu, alimualika Pezeshkian kufanya ziara rasmi na ulikubaliwa na kiongozi huyo.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Iran, IRNA, Pezeshkian alisema kila siku uhusiano kiuchumi, kitamaduni na mawasiliano yanazidi kuimarika kati ya pande mbili.

Kuimarika kwa uhusiano huo kunaangaliwa kwa mashaka na mataifa ya Magharibi, ambayo yanayachukulia kuwa mahasimu wao.

**DW**

## DRC, Rwanda kuanza mazungumzo mapya

**LUANDA, Angola**

MAWAZIRI wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Rwanda, wamekutana nchini Angola kwa ajili ya kuanza mazungumzo ya kumaliza vita.

Chini ya upatanishi wa Angola, viongozi hao watajaribu kutafuta suluhu ya ghasia inayoendelea mashariki mwa DRC, ambako jeshi la serikali linapambana na waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda.

Huo ni mkutano wa tano, ndani ya mwaka huu wakati mvutano ukiendelea kati ya nchi hizo mbili.

Mkutano kati ya mawaziri wa mambo ya nje wa Rwana na DRC, haukutarajiwa kufanyika kutokana na ule wa awali ulimalizika vibaya.

Mkutano wao wa mwisho uliofanyika katikati ya mwa Septemba, wajumbe wa Rwanda na DRC waliondoka bila kutoa taarifa rasmi au tarehe yoyote ya mkutano ujao.

Suala ambalo walishindwa kuelewana ni kuhusu mpangilio wa mpango wa kutenganisha vikosi vilivyopo mashariki mwa DRC.

Kwa upande mmoja, DRC inatakiwa kutokomeza kundi la FDLR, linaloundwa na Wahutu ambao waliohusika na mauaji ya halaiki nchini Rwanda.

Kwa upande mwingine, Rwanda inatakiwa kuondoa wanajeshi wake kwenye ardhi ya DRC.

**RFI**

# Wahimizwa kujitokeza uchunguzi wa afya bure

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewahimiza wananchi mkoani hapa, kujitokeza kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali yakiwamo ya moyo na maambukizi kwa njia ya mkojo, ili kupatiwa matibabu.

Akizungumza katika uzinduzi wa kliniki ya kibingwa ambayo inaendeshwa na serikali kwa kushirikiana na Ubalozi wa China nchini katika viwanja vya Stendi ya Zamani mjini Njombe, Mtaka alisema ni vyema viongozi wakahamasisha wananchi kujitokeza, ili kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kupata matibabu.

"Katika kampeni hii kuna madaktari bingwa, madaktari bobezi na kuna vifaa, kama una mgonjwa nyumbani ni vizuri kutumia fursa hii apate matibabu.

"Huduma hii ni bure, hakuna gharama ni miguu yako tu njoo ufanyiwe vipimo, kwa sababu dawa zipo na kama ni mgonjwa wa rufani utapatiwa," alisisitiza.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. Juma Mfanga, alisema; "Tutafanya uchunguzi hapa, lakini kama itahitajika upasuaji utafanyika hospitali ya mkoa ambako pia utakuwa ni bure." Dk. Mfanga alisema huduma nyingine za kibingwa zinazotolewa hapo ni zinazohusu watoto wenye matatizo ya mifupa pamoja na misuli, magonjwa ya ndani kama vile shinikizo la juu la damu, kisukari, kiharusi na matumbo.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema uhusiano wa kihistoria kati ya nchi hizo mbili umefanikisha kuleta timu ya madaktari bingwa 27, ili kutoa huduma za kibingwa kwa Watanzania.

# CHADEMA yamulika rushwa uchaguzi mitaa

**Na Mussa Mwangoka, MPANDA**



UONGOZI wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Magharibi, umeiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), kutofumbia macho vitendo rushwa katika kipindi cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Magharibi inayoundwa na mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora, Masanja Katambi, alisema juzi kuwa kuelekea katika uchaguzi huo, TAKUKURU inapaswa kuwa macho na kudhibiti vitendo vyote vya rushwa.

"Mimi niwasihi TAKUKURU wawe macho sana katika kipindi hiki cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwa kuwa ndicho kipindi rushwa inatamalaki. Tunahitaji kupata viongozi safi ambao ni chaguo la wananchi.

"Sasa wakati vyama vikijipanga na kushiriki uchaguzi huo, TAKUKURU ihakikishe inaweka mitego ya kuwabaini watoaji na wapokea rushwa," alisema.

Masanja alisema uzoefu unaonesha kuwa nyakati kama hizi, baadhi ya vyama vya siasa kuanzia mchakato wa ndani wa kuwapata wagombea hadi uchaguzi husika, baadhi ya wanachama wamekuwa wakitumia rushwa kitu ambacho hakipaswi kufumbiwa macho.

Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Katavi, Erasto Wegoro, pamoja kuunga mkono kauli hiyo, pia alisema upande wao wamejiandaa kikamilifu kushiriki uchaguzi huo kwa kuwa wana imani viongozi wengi watakaochaguliwa watatokana na chama chao.

Alisema hivi sasa CHADEMA ina muundo mzuri wa viongozi ngazi ya shina, matawi hadi taifa na wengi ni vijana, wasomi na wenye ushawishi kwenye jamii, hivyo ana uhakika watatoa ushindani mkubwa na kunyakua viti vingi kwenye uchaguzi huo.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, na mchakato wa awali wa uandikishaji kwenye daftari la makazi ulianza jana katika mitaa, vitongoji na vijiji kote nchini.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Bosi amtimua mfanyakazi ampate demu wake



**Na Adam Fungamwango**

LEO tunautazama wimbo uliopigwa na bendi ya OTTU Jazz, wana wa Msondo Ngoma uliofyatuliwa mwanzoni kabisa mwa miaka ya 2000.

Ni utunzi wa mwanamuziki TX Moshi William, ambaye alijaaliwa kipaji cha kuimba na kutunga. Hadi anafariki 2006, alikuwa ametunga karibuni robo tatu ya nyimbo za Msondo Ngoma. Kila albamu ilipotoka alikuwa na nyimbo tatu au nne, katika vile vibao sita vinavyorekodiwa.

Wimbo wenyewe unaitwa, 'Jesca'. Maudhui ya wimbo huu yanawakuta watu wengi, hasa wale ambao wanafanya kazi ofisi au kampuni moja na wake zao au wapenzi wao.

Yameshatokea sana huko nyuma, tumesikia habari nyingi sana juu ya wafanyakazi kunyang'anywa wake au wapenzi wao na mabosi zao.

Mbaya zaidi ni kwamba mtu na mke au mpenzi wake bosi wao ni huyo huyo mmoja, na wanafanya kazi ofisi moja, halafu anaonyesha mapenzi kwake.

Mara nyingi kinachotokea ni kwamba kama mwanamke atasimamia msimamo wake, au mwanaume kuonekana analinda sana mali yake, basi atahamishwa, au kutimuliwa kazi.

Mara nyingi uongozi una miiko na maadili yake. Lakini baadhi ya viongozi, mameneja, wakurugenzi, mabosi wa wale wanaosimamia ofisi wanakiuka miiko hiyo kwa tamaa za kimwili.

Binti anafanya kazi pamoja na mumewe au mpenzi wake ambao inawezekana wameahidiana kuoana, basi naye anamtaka, tena kwa nguvu, akitumia pesa, na madaraka aliyopewa.

Chochote atakachotamka hapo kitaonekana kiko sahihi kwa sababu ni bosi, kumbe nyuma ya pazia kuna tatizo.

Anaweza kusema jamaa mwenye mpenzi wake ni mvivu, jeuri, au akamsingizia chochote kile ili mradi tu amuweke kwenye mazingira ya kumhamisha au kumtimua.

Na hii yote kwa sababu anamtaka mpenzi au mkewe ambao wapo ofisi moja. Kama nilivyosema haya yalitokea huko nyuma, yanaendelea kutokea na yataendelea.

Wanamuziki wa zamani walinatunga vitu ambavyo ni vya uhalisia kwenye maisha. Kama kilitokea nyuma, kilatokea leo, na kitatokea vizazi hadi vizazi.

Kama halimkumpata mtu leo, kesho linangoja. Hebu tuangalie sasa mashairi ya wimbo huu.

> **Na hii yote kwa sababu anamtaka mpenzi au mkewe ambao wapo ofisi moja. Kama nilivyosema haya yalitokea huko nyuma, yanaendelea kutokea na yataendelea.**

"Jesca nilee mama, Jesca nishike moyo, nahitaji hekima yako oooh, Jesca yeyeee

Bosi wetu anaelewa wewe ni mpenzi wangu, ameamua nifutwe kazi hii, akupate wewe hee. Jesca nilee mama, Jesca nishike moyo, nahitaji hekima yako oooh, Jesca yeyeee. Bosi wetu anaelewa wewe ni mke wangu, ameamua nifutwe kazi hii, akupate wewe hee."

Hapa inaonesha kuwa mwanaume anahitaji msimamo wa mpenzi wake, kwani bosi ameshaamua atimuwe kazi kwa sababu ampate msichana huyo.

Bosi anaona kuwapo pale ofisini kwa jamaa, ni kama anamuwekea kiwingu katika harakati za kumpata msichana huyo.

Pamoja na kutimuliwa, jamaa bado anaendelea kumlilia mpenzi wake, alimtaka mpenzi wake aseme jambo moja, kama baada ya kutimuliwa, amemkubali bosi au vipi.

"Jesca mimi ninakupenda, kumbe bosi naye ni wako, Jesca mama, weka wazi

Jesca mimi ninakupenda, kumbe bosi naye ni wako, Jesca mama."

Mwanaume anamuuliza mpenzi wake, kumbe siku zote wanapendana, bosi naye alikuwa mtu wake? Akimtaka aweke wazi kama ilikuwa hivyo.

"Aaa Jesca, mpenzi wangu ee, wewe ni hakimu wa penzi letu, Aaa Jesca, mpenzi wangu ee, wewe ni hakimu wa penzi letu

Bosi wetu alitumia uwezo wake, bosi wetu alitumia cheo chake, na kuliteketeza penzi letu, na kuliteketeza penzi letu, na kuleta maumivu moyoni mwangu, na kuleta maumivu moyoni mwangu, Jesca, mama nalia eee."

Jamaa anamwambia Jesca kuwa yeye ndiye atakuwa hakimu wa penzi lao. Kama atabaki na yeye, au ataamua kumkubali bosi, kwani anatumia uwezo wake na cheo chake kulitekekeza, ikiwamo kuamua yeye afukuzwe kazi.

Jamaa analia kwani hataki kukosa mwana na maji ya moto. Akose kazi na mpenzi pia. Hapo Jesca ndiye mwamuzi.

***Tume meseji 0716 350534***

# HADITHI

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamuachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

# Nyuma ya Pazia-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**


"Unapafahamu Kinondoni Mkwajuni kituoni kama unatoka Mwananyamala, Makumbusho, au Kinondoni Morocco?" "Ndiyo napafahamu." Akaitikia. Sasa kama ukitoka hapo kuelekea Magomeni Makanya kabla hujafika si kuna bonde lile la Mkwajuni?" "Nalifahamu." Upande wa kushoto kama unaelekea huko ukipita daraja kuna miti mingi na mteremko mkali, nyumba zinaonekana zipo chini pamoja na miti!" "Ndiyo." "Na eneo hilo kama unatoka Kariakoo, au Kigogo, ukipita kwenye kituo cha Magomeni Kanisani, ukianza kuteremka bonde linakuwa linakuwa upande wako wa kulia, si ndiyo?" "Ndiyo."

"Basi lile eneo ndiyo tunataka utuwekee mzigo wetu pale, ulete kwenye kiroba, mkoba, sanduku, au shangazi kaja hiyo juu yako, sisi tunachotaka kiasi hicho cha pesa." "Kuna njia ya kuteremka kule?" Macky akauliza.

"Ndiyo, ukija mpaka pale kuna njia inashuka kule chini, kuna bonde kali, shuka taratibu utakutana na njia nyembamba na miti mingi na nyumba chache, utashuka hadi sehemu ambayo ni tambarare. Utakata kulia na hatua chache tu utakutana na mtu mnene zaidi kuliko yote iliyokuwa hapo. Chini ya mti ndipo utakapoacha mzigo. Cha kukukumbusha ni kwamba usimtume mtu yoyote. Changisheni wanandugu, mkope, mnyang'anye , lakini wewe ndiyo ulete kwa mguu wako. Nadhani umeelewa!" "Ndiyo nimeelewa." "Onyo nimesema uje peke yako na usijaribu ujanja wowote ule, usiwaambie askari polisi siku ya kuleta mzigo iwe siri yako. Kumbuka sisi tuna macho makali, masikio mapana, na mkono mrefu, ukiwaeleza polisi siku ya kuleta mzigo tutajua na inaweza kuwa hatari kwa mwanao." "Nimesikia." "Muda wa kuleta ni kuanzia saa tano usiku mpaka saa sita, na sisi ndiyo tutakuwa tunakupigia simu kukuuliza lini unaleta, wewe huwezi kutupigia kwa sababu hujui namba zetu. Kila siku tunatumia namba mpya na tutakayokupigia hatuitumii tena kwa ajili ya usalama wetu. Ujanja wowote utakuwa ni mauti kwa mwanao na kwako pia." Ilimaliza simu ile na kukatwa.

********************************

Pamoja na kuwa na hofu kwa kile alichoonywa, lakini Macky aliamua kuwaeleza askari juu ya kupigiwa simu na mtu asiyemfahamu akidai kuwa ndiye aliyemteka na kutaka kiasi hicho cha pesa.




**Ilikuwa ni saa nne asubuhi lilipofanyika zoezi hilo. Macky aliambiwa kuwa wakati wa kupeleka pesa, awasiliane kwanza na afande Tom, ambaye atakuwa kwenye gari la kawaida tu. Yeye ndiye atakuwa na mkoba huo wenye pesa. Atamfuata alipo na akumkabidhi mida ya usiku, masaa machache kabla ya kupeleka kunakohitajika.**

Akiwa Makao Makuu ya Polisi Kanda ya Kinondoni, hakuacha kitu. Alieleleza mpaka mbinu ambayo amedai watatumia ya kumpigia simu ili kujua kama amekamilisha pesa na atalipa lini.

Kamanda wa Kanda, aliwapa kazi hiyo askari polisi watatu ili kushughulikia suala hilo. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Tom Academy, Dickson Kisanga naye alikuwepo, pamoja na mzazi mwenzake Macky, ambaye jina lake ni Tunu. Siku hiyo Tunu alikuja peke yake. Hata hivyo pesa ambayo ilitakiwa ni nyingi sana kwa wahusika kiasi ambacho hata iweje ingechukua mwezi ili ziweze kupatikana kwa michango ya wanandugu, lakini zilitakiwa kwa siku saba tu.

Kwa hali hiyo, Jeshi la Polisi lililazimika kutoa kiasi hicho cha pesa kwa ajili ya kuzipeleka kwa waliomteka Macaire sehemu ambayo walitaka zipelekwe.

Zilitolewa kwa sababu ni mtego, wala zisingefika mikononi mwa wahalifu hao kabla ya kukamatwa.

Macky, alikabidhiwa vibunda kadhaa vya noti mpya kabisa kiasi cha Sh. Milioni 15. Baada ha kuhesabiwa na wote waliokuwa kwenye ofisi za jeshi la Polisi, zikiwekwa kwenye mkoba.

"Kama wakikupigia simu leo waambie kuwa umeshazipata na unaweza kuzipeleka leo hii hii usiku kule walikokuelekeza. Mengine tuachie sisi. Wakati huo tutakuwa tumeshalizunguka eneo lote na kuwatia mbaroni wahusika wote," alisema afande Chacha, ambaye ni mmoja wa askari watatu waliopewa kazi hiyo.

Ilikuwa ni saa nne asubuhi lilipofanyika zoezi hilo. Macky aliambiwa kuwa wakati wa kupeleka pesa, awasiliane kwanza na afande Tom, ambaye atakuwa kwenye gari la kawaida tu. Yeye ndiye atakuwa na mkoba huo wenye pesa. Atamfuata alipo na akumkabidhi mida ya usiku, masaa machache kabla ya kupeleka kunakohitajika.

Askari Polisi hawakutaka kumpa pesa zote hizo akakae nazo nyumbani kwa ajili ya usalama. Kwa kufanya hivyo hata wale watu wanazitaka hizo pesa wanaweza kumvamia na kumpora bila kumrejesha mtoto. Pia anaweza kuvamiwa na majambazi wengine na kuchukua pesa hizo ambazo zimechukuliwa tu kwenye kitengo cha Jeshi la Polisi kama chambo, lakini zina matumizi mengine.

Saa 10:00 jioni akiwa nyumbani kwake, simu yake ya mkononi iliita. Namba ilikuwa mpya, hivyo alijua ni wale wale. Hakukuwa salamu wala nini, jamaa walianza kuulizia pesa.

"Enhee, tuambie umeshapata pesa?" Lilikuwa ni swali la kwanza aliloulizwa. "Ndiyo nimezipata." "Umezipata wapi?" Lilikuwa ni swali ambalo hakulitarajia. Alisita kidogo kwa sababu hakujiandaa kujibu swali la aina hilo. Alikumbuka onyo alilopewa kutowaeleza askari polisi kuhusu suala hilo."Onyo nimesema uje peke yako na usijaribu ujanja wowote ule, usiwaambie askari polisi siku ya kuleta mzigo iwe siri yako. Kumbuka sisi tuna macho makali, masikio mapana, na mkono mrefu, ukiwaeleza polisi siku ya kuleta mzigo tutajua na inaweza kuwa hatari kwa mwanao." Alikumbuka Macky. Haraka wazo likamjiia, akajibu.

"Nimekopa kwa bosi wangu, nimweleza anikopeshe na atakuwa ananitaka taratibu kwenye mashahara," alijibu.


"Unajifanya mjanja eeeh!" "Hapana kiongozi, ni kweli." "Haya, fanya haraka leo saa tano mpaka sita kamili usiku, uulete mzigo sehemu tuliyokuambia." "Sawa mkubwa." Alipomaliza kujibu simu ikakatwa.

********************************

Ilikuwa ni saa nne usiku. Macky alikuwa amebeba mkoba wenye pesa. Hakuna yoyote aliyejua kama ulikuwa na kiasi cha pesa taslimu Sh. Milioni 15. Alitoka nyumbani kwake Manzese Argentina, na kupanda basi akashukia Magomeni Usalama. Aliambaa na barabara na baadaye kukata kushoto. Hakukuwa na watu wengi sana kama inavyokuwa mchana. Alipita maeneo ya Hospitali ya Magomeni, akapita pia Kanisa Katoliki, mita kadhaa baadaye alifika eneo la mwanzo wa bonde la Mkwajuni, kuelekea Kinondoni. Kulia kulikuwa na mteremko mkali na miti mingi kama alivyoelezwa. Alivuka barabara kwani alikuwa akitembea upande wa kushoto. Ni eneo ambalo halikuwa na mwanga wa kutosha. Taa za barabarani na giza vilishindana. Giza lilionekana kushinda mwanga kwa asilimia nyingi. Baada ya kuangalia sana aligundua kuwa kuna njia nyembamba ya mteremko mkali. Woga ulimuingia, lakini akikumbuka mtoto wake Macaire, alitengeneza ujasiri ndani ya moyo wake.

Akaamua kuteremka kwenye mteremko huo, huku akijizuia asiteleze. Na kila alipokuwa akishuka ndipo giza lilivyokuwa likishamiri.

*Itaendelea Jumapili*



# MJOMBA P DIDDY RUMANDE HADI MWAKANI

RAPA maarufu duniani, P Diddy ataanza kukabiliana na kesi zake zote zaidi ya 1000 kuanzia Mei 5, mwakani.

Mwanamuziki huyo raia wa Marekani, alikamatwa mwezi uliopita akituhumiwa kuwanyanyasa kingono wanawake zaidi ya 1000, ambao tayari wamewasilisha malalamiko yao mahakamani.

P Diddy ambaye jina lake halisi ni Sean Combs, bado ataendelea kusota rumande hadi mwakani kutokana na kufutiwa dhamana.

Hata hivyo mwenyewe amekana mashtaka hayo, huku timu yake ya wanasheria ikisema kuwa watu wamejitahidi sana kumharibia jina kwa kuvujisha mambo yake binafsi kwenye vyombo vya habari.


# *Profesa Jay aitaka tena Mikumi*

MSANII na mwanzilishi wa muziki wa bongo fleva nchini, Joseph Haule, maarufu kama 'Profesa Jay', amesema ana mpango wa kutaka kugombea tena ubunge kwenye Jimbo la Mikumi.

Mwimbaji huyo wa hip hop ambaye kwa sasa afya yake imeimarika baada ya kuugua, alikuwa mbunge wa jimbo hilo kwa tiketi ya CHADEMA, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.

"Nina mpango wa kwenda Jimboni Mikumi kugombea tena nafasi yangu ya ubunge. Wananchi wamekuwa na kilio kikubwa sana, kwa sababu wanakosa uwakilishi. Wamekuwa wakinipigia simu wakiniombea sana, wakiwa wanaamini mimi ni sauti yao, kwa sababu nilikuwa nikiwakilisha wananchi na si mimi mwenyewe na familia yangu," alisema msanii na mwanasiasa huyo mwenye kipaji kikubwa cha kuongea na kuhamasisha.

Afya yake imeendelea kuimarika siku hadi siku na kumfanya arejee kwenye majukumu yake ya kawaida ya kimuziki na kijamii pia.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVER KUIBOMOA LEVERKUSEN

LIVERPOOL inajiandaa kuivamia Bayer Leverkusen, kwa ajili ya kufanya mchakato wa kumsajili kiungo Mjerumani, Florian Wirtz, 21, mlinzi wa Uholanzi, Jeremie Frimpong (23) na kiungo wa kati wa Argentina, Exequiel Palacios (25) . ***(CaughtOffside)***

### ZUBIMENDI ATAJWA LIVER

LIVERPOOL pia wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Hispania, Martin Zubimendi, 25, kutoka Real Sociedad katika dirisha la usajili wa wachezaji la Januari. ***(Fabrizio Romano)***

### VILLA, NEWCASTLE VITANI

MLINZI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Joe Gomez, 27, anawaniwa na klabu za Aston Villa na Newcastle United. ***(Football Insider)***

### MURILLO AGOMBEWA ULAYA

REAL Madrid inamfuatilia mlinzi wa Nottingham Forest, Murillo, 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona na Bayern Munich kumpata Mbrazil huyo. ***(HITC)***

### GOMES SOKONI ENGLAND

KLABU za Newcastle United, Manchester United na Tottenham Hotspur ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Lille na Timu ya Taifa ya England, Angel Gomes, mwenye umri wa miaka 24. ***(GiveMeSport)***

### BARCELONA YASAKA KIPA

BARCELONA inatarajia kufanya mazungumzo ya dharura wiki hii kujadili iwapo watamleta golikipa mpya kuchukua nafasi ya mchezaji wao wa kimataifa wa Ujerumani aliyejeruhiwa, Marc-Andre ter Stegen. ***(ESPN)***

### DIAZ MAMBO SAFI

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia, Luis Diaz, 27, kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi kufikia mwaka 2027, baada ya kuwa na mwanzo mzuri wa msimu huu. ***(Football Insider)***

### LARSSON AGEUKA LULU

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt kutoka Sweden, Hugo Larsson, 20. ***(Fabrizio Romano)***

### UNITED YAMTAKA DIBLING

SOUTHAMPTON inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling, 18, kusaini mkataba mpya, huku Manchester United wakionyesha nia ya kutaka kumnunua nyota huyo. ***(GiveMeSport)***

### ATAJWA SUNDERLAND

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly, 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




## AGÜERO AAMUA KUISHTAKI BARCA

**Ni baada ya klabu hiyo kushindwa kutekeleza makubaliano ambayo...**

**BARCELONA,** Hispania

SERGIO Agüero, amewasilisha kesi mahakamani dhidi ya Barcelona ya madai ya euro milioni 3 kama sehemu ya fedha kwa kosa la kukatisha mkataba wake wa 2021, imefahamika.

**Agüero mwenye umri wa miaka 36, alijiunga na Barca kutoka Manchester City, kwa mkataba wa miaka miwili mwaka 2021, lakini alicheza mechi tano pekee kabla ya kulazimika kustaafu baada ya kupata matatizo ya moyo, wakati wa mchezo wa LaLiga dhidi ya Alavés.**

Alitangaza rasmi kustaafu mnamo Desemba, mwaka huo huo, na kufikia makubaliano na klabu ya kumaliza mkataba wake mapema.

Lakini ripoti inayoelezea hesabu za kifedha za Barca kwa msimu wa 2023-24 na kuonekana na ESPN imefichua mshambuliaji huyo wa zamani wa Argentina, alianzisha kesi za kisheria dhidi ya klabu hiyo mapema mwaka huu.

"Mnamo Mei 29, 2024, mchezaji wa zamani Sergio Agüero, aliwasilisha madai ya euro milioni tatu ambayo, kulingana na yeye, anadai kama sehemu ya makubaliano ya kumaliza uhusiano wake wa kikazi na klabu," ripoti hiyo imesema.

"Kufikia Juni 21, 2024, hakukuwa na makubaliano ya maridhiano kati ya wahusika. Klabu sasa inasubiri madai hayo kushughulikiwa na mahakama ya ndani kwa hatua inayofuata ya utaratibu."

Mzozo na Agüero ni mojawapo ya kesi tisa za kisheria zilizofafanuliwa na Barça katika sehemu ya ripoti inayoitwa 'Madai.'

Nyingine inafichua kampuni inayoitwa 'Scores Sports Management' inadai euro milioni 10 kwa jukumu lao katika uhamisho huo ambao ulishuhudia winga, Ousmane Dembélé, kuondoka Barca na kwenda Paris Saint-Germain kwa mkataba wa thamani ya euro milioni 50 mnamo mwaka, 2023.

"Mnamo Juni 18, 2024, klabu iliarifiwa kuhusu dai lililowasilishwa na Kampuni ya Scores Sports Management ikiomba euro milioni 10 kwa jukumu lao la upatanishi katika uhamisho wa Dembélé kujiunga na PSG," ripoti hiyo inaeleza.

"Kesi hiyo imesikilizwa na mahakama ya ndani kutokana na upinzani wa klabu na kutaka kupinga madai hayo."

Kesi hizo zimeorodheshwa na Barca kutokana na uwezekano wa athari zao za kifedha.



# VAN DIJK ALIA NA KADI NYEKUNDU YA KWANZA

**AMSTERDAM,** Uholanzi

VIRGIL van Dijk amesema "alikasirishwa" na uamuzi wa kupewa kadi ya kwanza nyekundu na kutolewa nje kwa mara ya kwanza kwenye maisha yake ya kuichezea Uholanzi katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Hungary kwenye mechi ya michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa iliyochezwa juzi.

Beki huyo wa Liverpool alipata kadi mbili za njano, ndani ya dakika tatu mwishoni mwa kipindi cha pili na kuelekea nyekundu.

"Kadi nyekundu ni mbaya, haikupaswa kutokea. Lakini nina hasira sana kuhusu kadi nyekundu ya kwanza," alisema Van Dijk akiiambia ESPN.

"Wanasema nahodha ndiye pekee anayeweza kuzungumza na mwamuzi. Nikatembea hadi kwake, lakini sio kwa njia mbaya, hata kidogo na nikaambulia kadi."

Kocha wa Uholanzi, Ronald Koeman, pia alishangazwa nahodha wake kuonyeshwa kadi hiyo.

"Wakati huo ulikuwa wa kufadhaisha," alisema Koeman akiimbia NOS.

"Sielewi, nadhani tulikubaliana nahodha anaweza kumpinga mwamuzi."

# Kinda wa Burnemouth anukia Arsenal

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal inapanga kuwasilisha ofa ya kumnunua beki wa kushoto wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Hungary, Milos Kerkez, mwenye umri wa miaka 20.

Mchezaji huyo alikuwa na msimu mzuri wa kwanza akiwa na Bournemouth na amekuwa chaguo la kwanza kama beki wa kushoto kwenye klabu hiyo.

Uchezaji wake tayari umezivutia klabu kubwa za Ulaya hasa zile za Ligi Kuu England, ambapo taarifa za karibuni zimemhusisha chipukizi huyo na Manchester United.

Beki huyo mchanga alijiunga na Bournemouth kutoka AZ Alkmaar ya Uholanzi Julai, mwaka jana.





# PSG yaipigia debe michuano ya FIFA

**ATHENS,** Ugiriki

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaïfi, amejitokeza kutetea muundo mpya wa Kombe la Dunia la Klabu la FIFA, akiwaambia wale ambao hawataki kushiriki mashindano hayo wasicheze.

Mashindano yaliyoboreshwa ya FIFA, yanatarajiwa kuanza nchini Marekani Juni 15, mwakani, yatahusisha timu 32 zitakazocheza kwa muda wa wiki nne.

Michuano hiyo imezusha ukosoaji kutoka kwa wachezaji kadhaa juu ya mafadhaiko ya ziada ambayo itaweka kwenye kalenda, na timu kama vile Manchester City na Real Madrid zimepangwa kwa msimu wa miezi 11 ikiwa zingesonga mbele zaidi katika dimba hilo.

Hata hivyo, Al Khelaïfi amesema klabu zimefurahishwa na michuano hiyo na itakuwa ikirudisha fedha zilizopotea kwa kuongeza mishahara ya wachezaji.

"Wachezaji au klabu zenye malalamiko zisicheze, ukiwa na malalamiko usicheze," alisema katika mkutano na wanahabari katika mkutano mkuu wa Jumuiya ya Klabu za Ulaya (ECA) mjini Athens, Ugiriki.

"Ni kweli tunatakiwa kuwaheshimu na kuwalinda wachezaji. Lakini klabu hazipo kwa ajili ya kutafuta fedha tu. Sio hivyo, hilo ni kosa. Tunajaribu kurejesha fedha kutokana na gharama zao. Mishahara inapanda na kupanda," alisema.

"Kalenda ni mada ya mjadala, ni wazi. Imekuwa hivyo kila wakati. Na, kusema ukweli, ninaamini ni muhimu kwa wahusika wote kukusanyika na kujadili, kwa njia ya mafanikio na kuona kile kinachofaa kwa kila mtu. Klabu zote zinataka kucheza Kombe la Dunia."

Mnamo Septemba, Al Khelaïfi, ambaye ni Mwenyekiti wa ECA, alikiri klabu zilikuwa zikipata maandalizi ya Kombe la Dunia la klabu "yakiwa na changamoto" lakini alisalia kujiamini katika mafanikio ya mashindano hayo.

"ECA inatambua kuna changamoto katika kuzindua muundo au dhana yoyote mpya, lakini tunaamini kwa dhati mashindano hayo yatafanikiwa."

## Yanga yasaka ushindi kisasa

INATOKA UK. 24

katika nafasi ya nne huku Simba yenye pointi 13, imeshinda michezo minne na kutoka sare moja.

Vigogo hao wawili wa soka nchini wote wametinga hatua ya makundi , Yanga ikishiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Simba yenyewe inapeperusha bendera ya Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Simba kushusha mlinzi mwingine

INATOKA UK. 24

wenye nguvu na wajanja na akina Mabululu (Cristovao Paciencia).

Kocha (Fadlu), amewaambia viongozi ana mabeki wazuri, lakini pia anahitaji aina hiyo ya beki, ambaye hapishani na mtu, kama ilivyokuwa kwa Joash Onyango kipindi chake yupo kwenye fomu, lakini huyu uwezo wake ni mara nyingi zaidi yake, kucheza RS Berkane siyo mchezo," kiliocheza chanzo chetu.

Wakati viongozi wakiwa katika mchakato wa kumwania beki huyo, inaelezwa huenda wakampoteza kipa, Ayoub Lakred, raia Morocco, anayetakiwa na Wydad Casablanca ya nchini kwao.

Taarifa zinasema nyota huyo wa zamani wa AS FAR Rabat, alisaini mkataba wa mwaka mmoja na Simba na ikifika dirisha dogo la usajili atakuwa amemaliza nusu ya mkataba wake.

Habari zinasema vigogo hao wa Morocco, wanamhitaji kwenda kusaidiana na kipa, Yusuf El Motie.

Hata hivyo, inaweza kuwa ni rahisi zaidi kwa Simba kuachana na kipa huyo, kwa sababu hajaonekana dimbani tangu kuanza kwa msimu kutokana na majeraha yaliyokuwa yanamkabili.

Kipa huyo aliondolewa kwenye mfumo wa usajili ya kimataifa TMS, nafasi yake ikachukuliwa na straika, Leonel Ateba, huku mwenyewe akiendelea kulipwa stahiki zake kama kawaida.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema kwa sasa hawezi kuzungumzia chochote kuhusu usajili wa dirisha dogo, kwa sababu wakati wake bado, badala yake anawaomba wanachama na mashabiki, macho yao wayaelekeze kwenye mchezo wa dabi utakaofanyika Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Tupo katika kipindi cha hamasa cha mchezo wetu dhidi ya Yanga, kwa sasa tuache kwanza, ila muda utafika, Desemba haipo mbali, kila kitu kitajulikana," alisema Ahmed.

# NGOGONGORO HEROES, RWANDA HATUMWI MTOTO CECAFA U-20

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inatarajia kuikaribisha Rwanda katika mechi ya Kundi A itakayochezwa leo, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Ngorongoro Heroes yenye pointi sita sawa na Sudan ndio vinara wa Kundi A wakati Rwanda iko katika nafasi ya nne, ikiwa na pointi mbili.

Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Boniface Mkwasa, amesema timu yake iko tayari kwa ajili ya mchezo huo na wataongeza umakini, kwa sababu Rwanda watashuka dimbani wakiwa hawana presha yoyote.

**Mkwasa alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu, lakini kikosi chake kitaingia tofauti kulingana na mpinzani wanayekutana naye.**

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mchezo wetu wa hatua ya makundi, tunajua hautakuwa mchezo rahisi, lakini tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi na kuongoza kundi letu," Mkwasa alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Rwanda U-20, Eric Nshimiyimana, amesema mechi hiyo dhidi ya wenyeji itakuwa ngumu, lakini amewaandaa wachezaji wake kucheza soka la ushindani.

"Haitakuwa mechi rahisi, tunajua Tanzania wanataka kujihakikisha tiketi ya kusonga mbele, lakini sisi pia hatutaki kupoteza, nimewakumbusha wachezaji kucheza kwa kuwaheshimu wapinzani," alisema kocha huyo na kiungo wa zamani wa APR na Amavubi.

Aliongeza amefanyia kazi mapungufu na anaamini wataingia katika mechi hiyo wakiwa imara.

Tayari Uganda na Burundi zimeshakata tiketi ya kucheza hatua ya fainali ya michuano hiyo, itakayofanyika Oktoba 18, mwaka huu na fainali ikichezwa siku mbili baadaye.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiwalani iliyopo Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mpira wa magongo kwenye Uwanja wa JKM Park jijini humo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tekeleza yalia na washambuliaji*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuchapwa mabao 3-1 na Maafande wa Mafunzo FC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa nje wa Amaan (Annex B), Kocha Msaidizi wa Tekeleza, Juma Salum, amesema washambuliaji ndio tatizo katika kikosi chake.

Tekeleza kutoka Pemba imepoteza mechi ya pili mfululizo kwenye uwanja huo na kuendelea kujiweka katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Salum, alisema timu yake bado inakabiliwa changamoto ya wachezaji wa eneo la mbele kutokuwa na uzoefu na hivyo wanapoteza umakini.

Kocha huyo alisema licha ya kufanikiwa kumiliki mpira kwa muda mrefu, lakini wanashindwa kutumia vyema nafasi wanazopata.

Aliongeza wataendelea kuwapa mbinu mpya, ili kuhakikisha hawapotezi pointi katika mechi nyingine tisa zilizobaki za mzunguko huu wa kwanza.

"Tunafanikiwa kuwanyang'anya mipira wapinzani wetu, tunatamba nao kwa muda mrefu, lakini wachezaji wanashindwa kupeleka mbele na kufunga, sijajua ni uoga au kupoteza umakini, najua timu yangu ni changa katika Ligi Kuu Zanzibar, tunawaomba mashabiki wawape muda wachezaji, ili kuzoea mikikimikiki ya ligi hii," aliongeza kocha huyo.

# Michezo

Jumapili Oktoba 13, 2024

Nipashe





Agüero kuishtaki Barca UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Kundi H dhidi ya DR Congo, ili kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

## Simba kushusha mlinzi mwingine

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imetajwa iko katika mazungumzo wa beki wa kati ya RS Berlane, Issouf Dayo, ambaye ni raia wa Burkina Faso, ili kumsajili kipindi cha dirisha dogo, kwa lengo la kuongeza nguvu kwenye kikosi chake.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya Simba zinasema baada ya kumalizana na Elie Mpanzu, benchi la ufundi, likiongozwa na Kocha Mkuu, Fadlu Davids, limewaeleza viongozi wanahitaji kujiimarisha zaidi, ili kufanya vyema katika hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Chanzo hicho kilisema Fadlu aliweka wazi anahitaji beki ambaye ni mrefu, mwenye nguvu na uzoefu wa michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Kwa sasa viongozi wetu wanaendelea na mazungumzo na menejimenti ya beki huyo, ili kupata saini yake, nafikiri itakuwa rahisi kidogo kwa sababu mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hivyo uhamisho wake hautagharimu ada kubwa sana," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 33 na mrefu futi sita na inchi mbili, ameonekana kumvutia Fadlu ambaye anahitaji awe na beki wa aina hiyo katika kikosi chake.

"Tuna walinzi lakini hatuna walinzi katili, ambao wanaweza kuwatisha mafowadi kwa umbile na hata uchezaji wa kutumia akili na nguvu pia. Tuna walinzi wazuri sana, lakini wote ukiwaangalia ni wale ambao wanatumia zaidi akili, linapokuja suala la nguvu zaidi inakuwa tatizo, nadhani atakuja kuwa suluhisho kwa mastraika wakorofi,

INAENDELEA UK. 23

# *Yanga yasaka ushindi kisasa*

## ●●● Yawaandalia usafiri 'rafiki' nyota wake ili kuiwahi dabi baada ya...

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha wachezaji wake wanarejea haraka ili kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mechi ya dabi, mabosi wa Yanga wameandaa utaratibu wa kuwarejesha mapema nyota waliokuwa kwenye timu za mataifa yao, imefahamika.

**Mechi ya watani wa jadi ya mzunguko wa kwanza ambayo Simba watakuwa wenyeji itachezwa Oktoba 19, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia gazeti hili jana, wameandaa utaratibu wa kuhakikisha wachezaji wao wote wanarudi nchini haraka na kwa njia rahisi, ili kujiepusha na uchovu wa kusafiri kwa muda mrefu ambao amedai huwa unawachosha wachezaji.

"Idara yetu ya utimamu kwa mwili imekuwa ikifanya mawasiliano na wachezaji wote kuhakikisha wanalinda miili yao na tunaangalia njia zote rahisi na nzuri kuhakikisha wanarudi mapema na salama, ili kuuwahi mchezo huo, wakiwa hawana uchovu.

Changamoto kubwa ambayo wachezaji wanaipata ni kusafiri, ukiangalia taratibu za kuunganisha safari za ndege kwenye jiografia ya bara la Afrika, mchezaji anatakiwa akae njiani kwa siku mbili, atoke nchi moja ya Afrika, aende mpaka Ulaya (Uturuki), akae saa 10 au 15 na pengine mpaka 20, halafu arejee tena Afrika, hii inafanya wachezaji kuwa na mchoko au fatiki, akifika badala ya kupumzika anatakiwa ajiandae na mchezo unaofuata wa klabu yake," alisema Kamwe.

Aliongeza hata makocha wanavyolalamika juu ya wachezaji wao kwenda kwenye vikosi vya timu za taifa, mara nyingi huwa ni usafiri na si kucheza mechi nyingi kwa muda mfupi.

"Waliopanga ratiba si watu ambao hawajui mpira, wapo sahihi kabisa, kila kitu kimepangwa ndani ya kanuni za soka na taratibu zake. Taratibu zinasema mchezaji anatakiwa kukaa saa 72 kabla ya kucheza mchezo mwingine, tatizo kubwa siku zote huwa ni usafiri tu, safari hii sisi tumeliangalia," Kamwe alisema.

Kuhusu mechi ya dabi, Kamwe alisema wameshazungumza na wachezaji wao, wanachohitaji ni kuzipata pointi tatu tu na si vinginevyo.

"Hakuna kombe la dunia pale, wala si fainali ya mashindano yoyote, ni mchezo wa Ligi Kuu tu, hata timu ipige visigino, kanzu, matobo au icheze mpira mzuri vipi, kinachotakiwa kwenye mchezo ule ni kuondoka na pointi tatu, kama hawatapata mashabiki hawatawaelewa, tumeshawaambia wachezaji wetu tunachohitaji ni ushindi wa mabao yoyote yale, hata ikiwa moja," aliongeza ofisa huyo.

Baadhi ya wachezaji wa Yanga waliokuwa kwenye timu za taifa, ukiachilia mbali Watanzania ambao wao wanarudiana na DR Congo hapa nyumbani, watakaosafiri ni Clatous Chama na Kennedy Musonda waliokuwa kwenye kikosi cha Zambia ambayo ilienda kucheza dhidi ya Chad wakati Stephane Aziz Ki, akiwa na Burkina Faso iliyoishindilia Burundi mabao 4-1, na Djigui Diarra akiwa na Mali wao walikuwa wanakutana na Guinea Bissau nyumbani na ugenini.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi watashuka katika mechi hiyo wakiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zao nne walizocheza na kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wako

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >